## Mwinyi asimulia mauaji ya kimbari Rwanda yalivyompa wakati mgumu

**Na Christina Mwakangale**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, anasema, katika uongozi wake kati ya masuala ya mambo ya nje yaliyompa wakati mgumu, ni mauaji ya kimbari nchini Rwanda.

Anasema eneo la Maziwa Makuu, hususan mgogoro katika nchi za Burundi na Rwanda, ulisababisha aitishe mkutano kutafuta amani kwa nchi hizo, Aprili 6, mwaka 1994 jijini Dar es Salaam.

Kwenye simulizi ya kitabu chake kiitwacho 'Mzee Rukhsa. Safari ya Maisha Yangu', Mzee Mwinyi, anasimulia namna alivyoweka jitihada za kutafuta amani na usalama kwa juhudi zake na kushirikiana na viongozi wenzake.

"Mojawapo ya mambo yahusuyo nchi za nje yaliyonisumbua sana wakati nikiwa rais ni matatizo ya maeneo ya Maziwa Makuu, ikiwamo ugomvi wa nchini Rwanda na Burundi, zaidi mauaji ya kimbari," anasema Mzee Mwinyi.

Anasema kwa kipindi cha miezi mitatu cha mauaji hayo, kuanzia Aprili hadi Julai, mwaka 1994, hawezi kukisahau na kuamua kuitisha mkutano ulioshirikisha serikali iliyokuwa ikiongozwa na Rais wa Rwanda, Juvenal Habyarimana pamoja na Cyprien Ntaryamira rais wa Burundi, wakati huo.

"Marais hawa wawili kila mmoja alikuja (Dar es Salaam) na ndege yake. Rais Habyarimana alikuwa amempa lifti balozi wetu katika nchi yake, Saleh Tambwe (kuja Tanzania). Walipokuwa wanarejea makwao, Rais Habyarimana ambaye ndege yake ilikuwa na kasi kubwa zaidi, aliamua kumpa lifti Rais wa Burundi, Ntaryamira...ndege iliyowawabeba marais hao ilitunguliwa."

Wote waliokuwamo kwenye ndege hiyo wakafa...ikazuka vita mara moja nchini humo na kufumba na kufumbua, Watanzania karibu 2,000 wakaenda ubalozini kuomba msaada wa dharura wa ulinzi na kurejeshwa Tanzania."

Mzee Mwinyi anaeleza namna alivyoshtushwa na vifo vya marais hao, kwa kuwa duniani tukio la viongozi wawili wa nchi kufa kwenye tukio moja, huwa ni nadra.

"La kusikitisha zaidi ni kwamba marais wote wawili walikuwa nchini mwetu, kutafuta suluhu na kukomesha mauaji yaliyokuwa yanaendelea katika nchi zao, kuleta amani, maelewano na ushirikiano...kilichokuwa kibaya zaidi...kifo cha Rais Habyarimana kuwa chanzo cha mauaji ya kimbari," Mzee Mwinyi anasimulia kwenye kitabu chake.

Mzee Mwinyi anasema kamati ya Umoja wa Mataifa iliyoanzishwa na kutoa taarifa yake Desemba 9, mwaka 1994, ilikadiria kwamba raia 500,000 waliuawa, ingawa uchunguzi uliofanywa na serikali ya Rwanda ulisema idadi ya vifo ilifikia watu 951,018.

Anasema historia ya Rwanda na Burundi, inabakia kuwa somo la kujifunza madhara ya ubaya wa ubaguzi wa kikabila, na kwamba ukoloni ulichangia kuandaa mazingira ya kushindwa kujitawala kwa amani na kuendelea.

"Tufanye kila tuwezalo kuua kabisa mbegu za ukabila zilizosalia na kujenga uchumi wa nchi zetu, kwa kuzingatia maslahi ya watu wetu, nchi zetu na bara letu," anasema Mzee Mwinyi.



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, akizungumza na Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula (WFP) nchini, Sarah Gordon Gibson, jijini Dodoma jana, kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na programu za chakula katika makambi ya wakimbizi yaliyopo nchini. **PICHA: WMNN**

# Kikwete azushiwa kifo

**Na Romana Mallya**

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, amezushiwa kifo na kusababisha taharuki na usumbufu kwa wanafamilia.

Mtoto wake, Ridhiwani Kikwete, jana alilazimika kutumia ukurasa wake wa Instagram kukanusha taarifa za uzushi huo akisema: "Baada ya kupokea simu na ujumbe mbalimbali, nimeona nitumie nafasi hii kuweka kumbukizi sawa.

"Mzee wetu na mzazi wetu Dr. @jmkikwete (Rais Kikwete) yupo salama wa afya nyingi sana.

Hana tatizo lolote kiafya na anaendelea na majukumu yake. Taarifa za aina yoyote ni za kipuuzi na za kupuuzwa."

Mapema mwaka huu, aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (sasa Makamu wa Rais), alikuwa miongoni mwa viongozi waliozushiwa vifo kipindi hicho ambacho Tanzania ilishuhudia vifo kadhaa vya viongozi.

Februari 19, mwaka huu, Rais Hayati Dk. John Magufuli, alilazimika kutoa ujumbe mahususi kwa wananchi kuepuka tabia hiyo ya kuzusha vifo vya viongozi, akisoma ujumbe mfupi aliotumiwa na Dk. Mpango aliyekuwa amelazwa hospitalini jijini Dodoma.

Wakati kukiwa na uvumi wa kilichodaiwa kifo cha Rais Kikwete, kiongozi huyo jana alionekana katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) akishiriki shughuli za chuo hicho ambacho yeye ni mkuu wake.

# Vikwazo vyaibuka Chato kuwa mkoa

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita mkoani Geita wamepinga wilaya mpya ya Busanda inayotarajiwa kuundwa kupelekwa mkoa mpya utakaoanzishwa wa Chato.

Madiwani hao wamesema ikiwa hilo litafanyika, Mkoa wa Geita utapoteza sifa kwa kubakiwa na wilaya tatu.

Wakichangia hoja hiyo wakati wa kikao hicho cha baraza maalum la madiwani, walisema ili mkoa uanzishwe mojawapo ya kigezo ni kuwa na wilaya zisizopungua tatu, hatua ambayo itatunyima sifa mkoa mama wa Geita kwa kubakiwa na wilaya tatu huku Chato ukiwa na wilaya sita.

Wakizungumza katika baraza hilo kuhusu wilaya mpya ya Busanda na kupelekwa katika mkoa mpya wa Chato kutokana na jiografia ilivyo, itakuwa ni kuwatesa wananchi wa eneo la Busanda ambao wao wanawawakilisha kutokana na umbali uliopo kutoka Busanda kwenda Chato.

Walisema kuwa iwapo wilaya hiyo italazimishwa kupelekwa katika mkoa mpya wa Chato watakuwa pia wanaua sifa za Mkoa wa Geita ambao ni mkoa mama utakaobaki na wilaya tatu ambazo zitakuwa Geita.

Diwani wa Bugulula, Elisha Lupuga, ambaye aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita wakati mchakato huo ukianza, alisema maamuzi ya madiwani yanapaswa kuheshimiwa kwani haiwezekani mkoa mpya uwe na wilaya sita halafu mkoa mama uwe na wilaya tatu, hatua itakayouathiri hata kiuchumi.

Mkurungezi Mtendaji wa Halmashauri ya Geita, Edith Mpenzile, akisoma taarifa kwa madiwani kuhusu maelekezo ya kuanzishwa kwa mkoa mpya, alisema idadi ya watu wanaotakiwa kuazisha mkoa inatakiwa iwe asilimia 3 ya idadi ya watu kitaifa.

Alisema kuiondoa Wilaya ya Busanda mkoani Geita na kuipeleka Chato, kutapunguza idadi ya watu, hivyo kuathiri kigezo cha idadi ya watu katika kuanzisha mkoa huo.

Aliongeza kuwa kijiografia katika kigezo hicho kamati ya fedha, uongozi na mipango imezingatia umbali wa wananchi, maeneo yote ya Wilaya ya Busanda yapo karibu na makao makuu ya Mkoa wa Geita ikilinganishwa na mkoa tarajiwa wa Chato.

Aidha, kamati hiyo iliangalia umbali kwa kuzingatia kilometa kwa wananchi wanaotoka katika Kata ya Butobela wanasafiri kilometa 83 kufikia makao makuu ya Mkoa wa Geita, wakati ikipelekwa mkoa mpya zitakuwa kilometa 195 kufika makao makuu ya mkoa mpya wa Chato.

Alifafanua hatua ya kisiwa cha Rubondo kwenda mkoa mpya pia wa Chato, ni kuathiri uchumi wa Halmashauri ya Geita Vijijini, hivyo kibaki katika halmashauri hiyo.

Mchakato unaoendelea wa uanzishwaji wa mkoa mpya wa Chato, ambao unalenga kuwa na wilaya sita za Chato, Bukombe, Ngara, Kakonko, Biharamlo pamoja na wilaya mpya inayopendekezwa ya Busanda, na mkoa mama wa Geita utabaki na wilaya tatu ambazo ni Geita, Mbongwe na Nyag'hwale. Wakati wa maziko ya Rais wa awamu ya tano, Dk. John Magufuli, Machi 26, mwaka huu kijijini kwake Mlimani, wilayani Chato, wazee wa wilaya hiyo, alimwomba Rais Samia Suluhu Hassan, kuendeleza mchalato wa kuifanya Chato kuwa mkoa, kama hatua ya kumuenzi Hayati Magufuli.

Hata hivyo, akijibu ombi lao, Rais Samia aliwataka kuendelea na mchakato huo kuona kama vigezo vya kuwa mkoa vitakidhi.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango, akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa kituo cha kudhibiti viumbehai waharibifu, Dk. Ladslaus Mnyome (kulia), kuhusu panya aliyepata mafunzo ya kufanya utafiti wa kugundua vimelea vya kifua kikuu na kugundua mabomu yaliyotegwa ardhini, alipotembelea maonyesho ya ufugaji katika Wiki ya Maadhimisho ya 17 ya Kumbukizi ya Hayati Edward Moringe Sokoine, katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Kampasi ya Moringe, mjini Morogoro jana. **PICHA: OMR**

# Serikali kujenga sanamu ya Sokoine

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imeridhia ombi la kujengwa kwa sanamu ya Hayati Edward Moringe Sokoine katika eneo la Wami- Luhindo (Dakawa), wilayani Mvomero alipopata ajali na kujengwa shule ya sekondari mchepuo wa sayansi kidato cha tano na sita kwa ajili kumbukumbu ya kihistoria.

Agizo hilo la serikali limetolewa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, wakati akihutubia wananchi na viongozi mbalimbali akifunga Wiki ya Maadhimisho ya Kumbukizi ya 37 ya aliyekuwa Waziri Mkuu, Hayati Edward Moringe Sokoine.

Makamu wa Rais alitoa agizo hilo kufuatia ombi lililowasilishwa na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigella, la kutaka eneo hilo alilopatia ajali Hayati Sokoine lijengwe sanamu ya kumbukumbu kwa ajili ya wananchi na vizazi vijavyo kupata historia ya kiongozi huyo.

Akiwasilisha salamu za mkoa huo, Shigella alisema wakati akiwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana, alisema eneo alipopata ajali Hayati Sokoine lilikuwa kando ya shamba linalomilikiwa na Umoja wa Vijana (UVCCM), Mkoa wa Morogoro.

Alisema uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Morogoro, wakati huo waliwasilisha ombi la kupewa eneo hilo kwa ajili ya ujenzi wa mnara na Shule ya Sekondari ya Kumbukumbu ya Sokoine ambayo tayari imeshajengwa.

Pia, waliomba serikali igharamie ujenzi wa sanamu katika eneo hilo ili kuweka alama au kumbukumbu kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho ili waweze kwenda kupata maelezo katika eneo hilo.

Akijibu ombi hilo, Makamu wa Rais alimwagiza Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, kuwa mratibu wa mchakato wa ujenzi wa sanamu hiyo akishirikiana na wizara nyingine zinazohusika na suala hilo.

Alisema kuwa wakati anapata mwaliko wa kuwa mgeni rasmi alikuwa anatafuta maandiko ya historia na mchango wa Hayati Sokoine katika maktaba, lakini hajaweza kuipata na alifanikiwa kuipata kwenye kumbukumbu zilizopo bungeni ambazo ni machapisho machache yaliyoandikwa na waandishi wa habari.

Makamu wa Rais aliagiza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, kuandika kitabu cha historia ya Hayati Sokoine baada ya kuwasilishwa ombi la familia yake ili kitumike na wananchi kujua mchango wake katika maendeleo ya taifa lao wakati wa uhai wake.

Awali msemaji wa familia na Mwenyekiti wa Mfuko wa Sokoine, Lemburis Kipuyo, alisema wanaishukuru serikali kwa kumuenzi Hayati Sokoine pamoja na Chuo Kikuu cha Sokoine kutambua mchango wake kwa kuanzisha na kuendeleza kumbukizi ambazo zinaleta manufaa katika jamii.

Naye Waziri Profesa Ndalichako, alisema amepokea maelekezo ya Makamu wa Rais kuhusu ujenzi wa sanamu hiyo na kumwagiza Katibu Mkuu wake, Dk. Leonald Akwilapo, kuanza mchakato wa ujenzi huo kwa kushirikiana na wizara nyingine.

# Ombaomba Dar es Salaam kurudishwa makwao Juni

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amewataka ombaomba wote walioko katika mkoa huo waende kujisajili majina yao, na itakapofika mwezi ujao warudishwe makwao.

Makalla amesema lengo la hatua hiyo ni kuondoa tatizo la msongamano wa watu katika Jiji la Dar es Salaam.

Alitoa maagizo hayo jana, ambapo aliongeza kuwa Dar es Salaam kumekuwa na tatizo la msongamano mkubwa wa ombaomba, na kwamba wengi wao ni watu wanaokimbia katika vijiji vyao na kukimbilia pasipo kuwa na kazi wala sehemu maalumu ya kufikia.

Alisema baadhi ya watu hao wamegeuza kuomba kama kazi ya kuwaingizia kipato, jambo ambalo si sahihi kwani wanasababisha usumbufu kwa wakazi na wageni wengine wanaoingia jijini humo.

"Ombaomba wote kwa hiari yenu, andikisheni majina na vijiji mlivyotoka, katika ofisi ya mkuu wa mkoa, na ifikapo mwezi Juni wote tutawasafirisha na kuwarudisha vijijini kwenu," alisema na kuendelea:

"Na ofisi yangu itagharamia gharama zote za usafiri mpaka makwao, ili kuondoa malalamiko ya wale wanaosema kuwa hawawezi kurudi kutokana na nauli."

Pia alitoa maagizo kwa wakuu wa wilaya kufanya msako wa mawakala wanaowasafirisha watu na kuwaingiza katika jiji hilo na kuwatumia kama njia ya kuwaingizia kipato, kwa kuwafanyisha kazi ya kuomba mitaani.

Alisema viongozi wa serikali za mitaa wafuatilie watu wote wanaoingia katika mitaa yao na kuwatambua, ili kudhibiti na kuondoa mzizi wa ombaomba wanaoingizwa katika jiji hilo.

"Wakuu wa wilaya, watendaji kata na viongozi wa serikali za mitaa anzisheni operesheni kali ya kuwasaka mawakala wote wanaoingiza ombaomba katika mkoa wetu, na tukiwabaini hatua kali zichukuliwe dhidi yao.



RIPOTI MAALUM

# Ijue siri mishahara watumishi wa umma kutopandishwa miaka sita

## •Hizi hapa hoja zinazoibua vikwazo

Na Sanula Athanas

KUNA mgongano wa hoja unaoendelea kwa muda mrefu kati ya mwajiri na mwajiriwa serikalini, ingawa kwa sura pana ni hadi sekta binafsi ambako ndiko kumeshika mapana ya uchumi nchini.

Kila upande unaohusiana na hoja hiyo, kuanzia wanaoguswa moja kwa moja na walio nayo kwa jirani, unawasilisha utetezi uliobeba mashiko kwa namna yake.

Ni kwa namna gani? Wakati mwajiriwa wa serikalini analia kutopatiwa haki yake ya kupandishwa cheo kwa muda mrefu, mwajiri anakiri ukweli huo, lakini kwa upande wa pili wa shilingi anasimama katika tafsiri 'haiwezekani kwa sasa kutokana na ugumu wa uchumi'.

Je, kupanda cheo kuna maana gani? Sheria ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2003 inatoa tafsiri kwamba: "Kupanda cheo ni kutoka ngazi moja kwenda kwenye ngazi ya juu yake kikazi".

Tafsiri hiyo yenye ufafanuzi katika Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009, inadokeza kuwa ni mabadiliko yanayoendana na ongezeko la mshahara kwa mnufaika.

Miongozo hiyo ya kisheria inaorodhesha vigezo muhimu vya kufikia uamuzi wa upandishaji vyeo na yanayoambatana nayo, ikijumuisha kuwapo nafasi zilizo wazi na zimeidhinishwa kisheria au kiutaratibu.

Vingine ni bajeti kuruhusu uwezekano huo, mlengwa kuwa na sifa ya utendaji kazi unaokidhi mahitaji kwa mujibu wa Tathmini ya Wazi ya Utendaji Kazi (OPRAS) na sifa hitajika kwa nafasi anayoelekezwa.




Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere.

### MVUTANO ULIPO

Wakati pande zote (mwajiri na mwajiriwa) wanakubaliana na vigezo vilivyopo, bado utekelezaji wake umebaki mgumu, kila mmoja ana utetezi wake anaouamini uko sahihi.

Hadi sasa ni hoja inayochukua sura pana, huku ulingo wa siasa uliobaki kando kwa muda, nao ukiingia, ikiwamo bungeni.

Watumishi wa umma kupitia mwakilishi wao, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) kwenye maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Kitaifa mwezi huu jijini Mwanza, Kaimu Katibu Mkuu, Said Wamba, alilalamika kutimu miaka sita pasipo kada hiyo kupandishwa vyeo na mishahara.

Ndani ya hafla hiyo, Rais Samia Suluhu Hassan, akawarejeshea ufafanuzi akikubaliana nao, lakini akiwaanikia uhalisia uliopo kwamba haiwezekani kwa sasa na akawaahidi kuliangalia hadi maadhimisho yajayo.

"Kwa miaka sita watumishi wa umma hawajaongezwa mishahara yao na wale wa sekta binafsi mishahara yao haijaongezwa kwa miaka minane sasa," Rais Samia alisema siku hiyo.

Hoja hiyo ya Mkuu wa Nchi inatetewa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiwa na ufafanuzi kuwa sehemu kubwa ya bajeti ya nchi inaelekezwa kugharamia madeni na mishahara ya watumishi wa umma.

Dk. Mpango ambaye ni mwanazuoni mchumi kitaalamu, aliyetumikia mashirika ya fedha kimataifa na pia kuwa Waziri wa Fedha na Mipango, anasema makusanyo ya nchi ni wastani wa Sh. trilioni 1.3 kwa mwezi na matumizi, wastani Sh. bilioni 600 hulipa madeni ya serikali huku mishahara ikichukua Sh. bilioni 550 katika muda huo.

Kiasi kidogo kinachobaki (takribani Sh. bilioni 150) kinatumika kugharamia huduma kama vile elimu, matibabu ya wazee na upanuzi wa miradi ya afya.

Muda mfupi baada ya kuapishwa kuwa Makamu wa Rais, Dk. Mpango aliitaka Mamlaka ya Mapato (TRA) kuongeza jitihada katika ukusanyaji wa mapato ili wafike wastani wa Sh. trilioni mbili kwa mwezi.

### ANGALIZO LA CAG

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, anatahadharisha kuwa hali hiyo ikiendelea, kutakuwa na utendaji duni miongoni mwa watumishi.

Katika ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2019/20 iliyowasilishwa bungeni mwezi uliopita, CAG Kichere anabainisha kuwa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 zinataka tarehe ya kupandishwa daraja ya mtumishi wa umma iamuliwe na mamlaka sahihi.

"Kinyume cha kanuni hizo, nilipitia mafaili ya watumishi pamoja na mfumo wa LAWSON wenye taarifa mbalimbali za watumishi na kubaini kuwa watumishi 7,992 katika mamlaka 14 za serikali za mitaa hawakupandishwa madaraja ingawa walikuwa na sifa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma.

"Kushindwa kupandisha madaraja na kutoa nyongeza ya mishahara kwa wakati kwa watumishi wa umma husababisha utendaji duni katika utoaji wa huduma na hii huhatarisha nia njema ya serikali ya kutoa huduma bora kwa wananchi," CAG anatahadharisha.

### HOJA BUNGENI

Nje ya ulingo wa wanaodai, Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye (CCM), anabeba bango la kilio cha wafanyakazi, akiwatetea kwamba ni muda mrefu wamesahaulika stahiki zao.

Pendekezo lake bungeni kuwatetea watumishi wa umma ni kuitaka serikali kuunda tume kuchunguza undani wa kusahaulika huko, kupunjwa mafao na stahiki zingine rasmi.

Ni hoja inayopatiwa sehemu ya ufafanuzi nje ya Bunge, Mwenyekiti wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Jayne Nyimbo-Taylor, akidokeza undani wa magumu yanayowakabili, akitaja mzigo wa mlundikano wa kodi.

Mwakilishi huyo wa kada ya waajiri nje ya serikali, anapendekeza haja ya kuwapo umakini katika marekebisho ya sheria ili yasiathiri uendeshaji taasisi kwa waajiri.

Vilevile, waziri mwenye dhamana na utumishi wa umma, Mohamed Mchengerwa, katika majibu yake bungeni ndani ya kipindi mfupi tangu kuteuliwa kushika nafasi hiyo, anatoa faraja kufanyia kazi hoja zenye sura ya kilio cha utumishi kwamba kutafanyika mapitio ili kutoa haki kwa wanaostahili.

### KIKWAZO CHA KIHISTORIA

Hata hivyo, hilo si suala geni. Ikirejewa Rais mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, katika kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', anakiri kadhia hiyo imo katika yaliyoupa ugumu uongozi wa nchi.

Mwinyi analitaja suala hilo kuirithi nchi tangu zama za mtangulizi wake, Mwalimu Julius Nyerere, aliyetoka nalo mwaka 1980, naye (Mwinyi) akilikuta lina miaka mitano.

"Ili kukabiliana na kushuka kwa uzalishaji na tija kwenye sekta ya umma, kwenye sherehe za Siku ya Wafanyakazi Duniani, Mei Mosi mwaka 1980, CCM ilitangaza sera mpya ya tija na kusema kuwa sasa wafanyakazi watalipwa kulingana na matokeo.

"Kwa maana hiyo, iwapo kiwanda cha umma kitapata hasara, menejimenti na wafanyakazi hawatakuwa na haki ya kulipwa nyongeza ya mshahara au kupandishwa vyeo, lakini bonasi zitalipwa pale ambapo kiwanda kimeongeza uzalishaji, tija na faida," Mwinyi anasema.

Katika kitabu chake hicho kilichozinduliwa na Rais Samia mwezi huu, Mwinyi anabainisha kuwa ili kutekeleza maagizo hayo ya CCM, serikali ilitoa Waraka wa Serikali Na. 1 wa Mwaka 1981 na kisha ikatunga Sheria ya Baraza la Tija la Taifa.

•ITAENDELEA KESHO

HABARI KITAIFA

# Ufafanuzi kilimo cha bangi nchini

**SERIKALI imesema haina mpango wa kuruhusu kilimo cha bangi nchini kwa kuwa bidhaa hiyo ni miongoni mwa dawa za kulevya.**

**Jana, Nipashe ilimnukuu Kaimu Kamishna Kitengo cha Huduma za Sheria wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya, Christina Rwehabuza, akibainisha kuwa kumefanyika marekebisho ya sheria ili kuruhusu bangi kutumika katika masuala ya tiba na utafiti.**

**Hata hivyo, uongozi wa juu wa mamlaka hiyo ulisisitiza jana kuwa kamwe Tanzania haitaruhusu kilimo hicho, kwa bangi ni haramu na kwamba nchi inayo mazao mengi ya biashara yanayotosha kuiingizia mapato.**

**Mhariri**

# Tiketi kivuko cha Magogoni kielektroniki

**Na Maulid Mmbaga**

WAKALA wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) imezindua mfumo mpya wa ukataji tiketi kwa njia ya kielektroniki katika Kivuko cha Magogoni na Kigamboni jijini Dar es Salaam utakaotumia kadi.

Akizungumza katika uzinduzi wa mfumo huo uliofanyika jana katika eneo hilo, Mtendaji Mkuu wa TEMESA, Japhet Massele, alisema mfumo wa N-Card utasaidia kupunguza msongamano katika kivuko hicho, kwamba unatoa huduma kwa haraka tofauti na uliokuwa ukitumika awali.

Alisema Mfumo wa N-Card unafanya kazi kwa kutumia teknolojia ya NFC, ambayo inamtaka abiria kuwa na kadi hiyo inayopatikana kwa gharama ya Sh.1000 na baada ya kununua ataweka fedha kupitia wakala wa N-Card au mitandao ya simu kuanzia Sh. 500 na kuendelea.

Massele alisema: "Huduma hii inapatikana katika vivuko vyetu vyote vya Magogoni na Kigamboni na juhudi zinaendelea ili kuhakikisha kuwa tunaongeza wigo wa abiria kuweza kujiwekea salio kwa kutumia benki na mitandao ya simu iliyobakia."

Aliongeza: "Abiria mwenye kadi yenye salio akifika kivukoni atagusisha kadi yake kwenye geti na kukatwa nauli stahiki ya Sh. 200 na ataweza kupita, kitendo hiki kinatumia sekunde moja kutokana na kuwa na mageti yenye kasi kubwa ya kufungua na kufunga, hivyo yanaweza kuhudumia idadi kubwa ya abiria kwa muda mfupi na kuondoa msongamano."

Aliongeza kuwa kwa sasa mifumo yote miwili wa tiketi za karatasi na kadi zitaendelea kutumika hadi hapo mfumo wa kielektroniki utakapozoeleka kwa abiria.

Aidha, alisema mfumo huo umeonyesha mafanikio kwa sababu umesaidia kwa asilimia kubwa kuondoa tatizo la abiria kupanga foleni mbili ya kununua tiketi na ya kuruhusiwa kuingia eneo la kusubiri kivuko.

Alisema TEMESA imesimika mageti mawili pande zote mbili za vivuko na inatarajia kubadilisha mageti yote ya zamani na kuweka mapya ili kurahisisha huduma hiyo kufanyika kwa ufanisi zaidi.

"Napenda kuwatoa hofu wananchi hasa wale ambao ni wageni kuwa mifumo yote miwili itaendelea kutumika mpaka hapo usimikaji wa mageti yote utakapokamilika.

"Kwa kuwa teknolojia hii ni mpya TEMESA kwa kushirikiana na NIDC inaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi ya mfumo huu wa kadi ili kuwaondolea changamoto ya kujua sehemu ya kupata kadi, kuweka fedha na namna ya kujua salio lililobaki kenye kadi," alisema Massele.

Massele alisema: "Abiria akipata changamoto yeyote ya kadi anaweza kuwasiliana na watoa huduma wetu waliopo katika vivuko vyetu na pia kwa kupiga simu namba 0800 11 01 50 kwa msaada zaidi na huduma hiyo ni bure."

# Bunge lapata dawa uboreshaji wa mifugo

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, imetoa mapendekezo manne ya uboreshaji wa sekta hizo kwa mwaka ujao wa fedha, lengo kuu likiwa ni kuwanufaisha wananchi wa kipato cha chini.

Akiwasilisha maoni na mapendekezo ya kamati hiyo jana bungeni, Mwenyekiti wake, Dk. Christine Ishengoma, alisema kubwa ni kukamilisha maboresho ya sera, sheria za uvuvi na mifugo kwa kuwa kamati imebaini kuwapo malalamiko kutoka kwa wadau. Aliwataja wadau hao ni wafugaji, wavuvi, wafanyabiashara wa samaki, mawakala wa biashara ya uvuvi, wamiliki wa viwanda vya kuchakata samaki na mazao ya mifugo.

"Msingi wa malalamiko yaliyopo ni kukosekana kwa mazingira bora na yenye tija katika shughuli za biashara ya mifugo na uvuvi kutokana na sera, sheria na kanuni zinazosimamia sekta hizi kutokuwa rafiki na baadhi kupitwa na wakati," alisema.

Dk. Ishengoma alisema kamati inapendekeza kuimarishwa kwa bajeti inayotengwa kwa ajili ya sekta ya mifugo na uvuvi, kutokana na umuhimu wake katika ukuaji wa uchumi.

"Takwimu zinaonyesha Tanzania ina ng`ombe takribani milioni 30.5 idadi ambayo inaifanya Tanzania kuwa nchi ya tatu kuwa na ng`ombe wengi barani Afrika baada ya Ethiopia na Sudan. Pamoja na wingi huu wa mifugo bado sekta ya mifugo haijatumika kikamilifu katika kuinua Pato laTaifa na kumsaidia mfugaji kuondokana na umaskini," alisema Dk. Ishengoma.

Dk. Ishengoma alisema mwaka wa fedha 2021/22, sekta ya mifugo imetengewa Sh. bilioni 16.8 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Alitaja pendekezo lingine ni uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu, alisema uchumi wa bluu ambao unajulikana kama uchumi wa bahari unafungamanisha kwa pamoja sekta za uvuvi, ufugaji samaki, ujenzi wa viwanda vya samaki, na matumizi bora ya rasilimali za bahari.

Vilevile, alisema licha ya Sh. bilioni 50 kutengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi, alisema ni vyema fedha hizo zikatolewa kwa wakati ili utekelezaji wa ujenzi wa bandari ya uvuvi uweze kuanza.

Dk. Ishengoma alitaja pendekezo lingine ni kuimarisha usimamizi wa nyanda za malisho nchini, alisema pamoja na dhamira hii njema, bado mashamba ya malisho yanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo uhaba wa maji kwa ajili ya kunyweshea mashamba ya malisho.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuamke kusaka majibu kulikoni matukio watoto kujiua yanashamiri

**KATIKA** maisha ya kijamii ndani ya mustakabali wa kila aina, dhana ya ulinzi na usalama wa mtoto huwa haina mjadala. Ana thamani ya leo, kesho pia anathaminishwa kwa taifa na maisha ya kesho.

Ni mantiki inayokamata kila kona. Kisheria ambako nchini kuna iliyo mahsusi za kumlinda mtoto wa Kitanzania, maudhui yake yote yanasimamia kulinda na kukuza thamani ya mtoto huyo.

Vitabu vitakatifu vya kiimani, vyote kwa jumla vinaangukia humo katika namna vinafafanua thamani ya mtoto, hata kufunga mjadala wa haja ya heshima na ulinzi wa mtoto.

Ziada ya hiyo, kuna la kipekee kwamba uhusiano kati ya mtoto na mzazi ni wa mzizi mrefu na hakuna asiyefahamu hilo lililo bayana, katika tafsiri zote zilizoko.

Ndani ya mustakabali huo imekuwa ikijitokeza matukio ya watoto wanafunzi kujiua, tena katika maeneo mbalimbali, hali inayotokana na picha, kuna mustakabali mpana wa matukio hayo.

Kwa kurejea hilo, mathalan ndani ya wiki kadhaa sasa zisizotimu jumla ya mwezi mmoja, mkoani Ruvuma kuliripotiwa binti mwanafunzi wa shule ya sekondari alijinyonga hadi kufa, tena kwa kumtoroka mlezi wao shuleni walipokuwa wote.

Ni taarifa inayohuzunisha wengi, kulikoni mwanafunzi mdogo na taifa la kesho anakatisha maisha kwa kukusudia tena katika mazingira tata ya namna hiyo.

Kabla haijapita wiki hiyo ya huzuni, lingine juzi tu kukaripotiwa taarifa inayofanana na mkasa wa binti wa Ruvuma, wasafari hii anasoma shule ya msingi wilayani Kibaha, naye kajiua katika namna inayofanana na mkasa wa dada yake wa Peramiho, Ruvuma.

Huenda kuna mengi ya namna hiyo katika kipindi kisicho kirefu yanatokea watu kujiua. Hiyo inajenga ujumbe huenda kuna mwenendo au tatizo nyuma ya pazia, hata inasababisha mfumo wa maisha kujaa matendo.

Hapo inajenga ujumbe gani? Jibu la kwanza, ni jamii kote anakohusika na kwa ujumla kuanza kutafakari mantiki na msukumo ulioko nyuma yake. Je, ni aina ya tabia, mfumo wa mashamba, au utamaduni mpya?

Inaeleweka mikasa na mambo mabaya katika jamii, si jambo jipya. Ila kanuni iliyoko mabaya hayaachwi pasipo kushughulikiwa kwa namna yoyote ile. Inatakiwa hatua ichukuliwe kurekebisha kuelekea kwenye mema, ambayo ni amani, utulivu na maendeleo.

Tunajua kuna miongozo ya kijamii kuanzia familia, ustawi wa jamii katika taasisi binafsi na za umma na mengine mengi yenye wajibu wa kurekebisha.


Jamii nayo kushukia ngazi ya familia na ukoo, wanakopatikana waathirika hao, wana nafasi yao katika hilo kwa kuchukua hatua stahiki, ikiwamo kutoka ndani ya nyumba za imani.

Kunatakiwa kuchukuliwa hatua za kukabili mwenendo huo ambao haubebi haiba nzuri kimantiki hata kidogo. Inawezekanaje?

Rais Julius Nyerere mwaka 1964, ambao una mengi yaliyoamuliwa kitaifa na yanayotekelezwa hadi sasa, aliishauri umma kwa kauli ifuatayo: "Inawezekana, timiza wajibu wako" kwa maana kila mmoja ashiriki kukabili walakini ulioko kwa nafasi yake, atasaidia mafanikio.

Hivyo kwa hili la taifa ya kujikuta inashuhudia vifo vya watoto, ni vyema kila mmoja atimize wajibu wake kuanzia na kujiuliza 'ni kwanini?" sambamba na kuipatia majibu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Tusaidie watoto wetu waende shule, siyo kufanya biashara

**HIVI** sasa ni wazi kwamba, wimbi la watoto wenye umri wa kwenda shule, lakini wako mitaani wakifanya biashara ndogo linatakiwa kupatia ufumbuzi wa kudumu, ili kuepuka kuwa na taifa la baadaye lenye watu ambao hawajasoma.

Kuna sababu mbalimbali ambazo huwa zinatajwa kusababisha uwepo wa watoto wa mitaani na hata wengine kuangukia kwenye biashara ndogo kama kuuza karanga, pipi, sigara, biskuti na nyingine kadhaa.

Miongoni mwa sababu hizo ni kutengana kwa wazazi wao au wote kufariki dunia na hivyo kuwalazimisha kutafuta maisha kwa kufanya biashara ndogo kwa lengo la kujiingizia kipato cha kuwawezesha kujihudumia.

Katika mazingira hayo, wapo baadhi ya watoto wenye umri wa kwenda shule ambao husimama kandokando ya barabara kuomba msaada wa fedha na wengine kuosha vioo vya magari kwa ujira kidogo.

Watoto wa aina hiyo wako katika maeneo mbalimbali ya mijini, ikiwamo Dar es Salaam, anakotafuta rikizi kwa njia hizo, hali inayosababisha wakose elimu ambayo ingeweza kuwasaidia katika maisha yao ya baadaye.

Bila kuwapo hatua madhubuti za kukabiliana na mazingira hayo, kuna uwezekano wa kuwa na vijana ambao hawatakuwa na faida kwa taifa lao la baadaye, ingawa vijana ni taifa la kesho.

Hivyo, wadau wote wakiwamo wanaohusika na ustawi na jamii, wanapaswa kuwasaidia kukomesha mtindo huo, ili watoto wenye umri wa kwenda shule wasome, badala ya kurandaranda mitaani kuomba msaada au kufanya biashara ndogo.

Nashukuru Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ameshaliona tatizo hilo na kupiga marufuku watoto na vijana wenye umri wa kwenda shule kufanya biashara kwenye vituo vya mabasi nchini. Ameagiza mamlaka husika kudhibiti mtindo huo. Hivyo, Waziri Mkuu anawataka wakurugenzi wa halmashauri kusimamia utekelezaji wa agizo hilo la kuwaondoa kwenye maeneo hayo watoto na vijana wenye umri wa kwenda shule.

Agizo lake ni kwamba, akikuta wanafunzi bado wanaendelea kufanya biashara kwenye stendi za mabasi, maana yake ataichukulia hatua halmashauri husika kwa kuwa zinatakiwa kuhamasisha wanafunzi kwenda shule.

Hapo ninasema, itakuwa ni hatua nzuri iwapo wahusika na wadau wengine watachukulia marufuku hiyo kwa uzito wake ili watoto na vijana wadogo wanaotakiwa kuwa shule wasiendelee kujihusisha na biashara.

Ni vyema, mamlaka za ustawi wa jamii wakafuatilia kiini cha watoto kukimbia kutoka nyumbani kwao na kwenda kuishi mitaani au kufanya biashara ndogo katika vituo vya mabasi badala ya kuhudhuria masomo shuleni.

Inawezekana wapo watoto wanaotumwa na wazazi kufanya biashara kutokana na kwamba familia haina uwezo kiuchumi, hivyo wanashirikishwa katika biashara hizo ndogo kupata fedha za kujikimu majumbani. Hata hivyo, bado haikubaliki kuwa mbadala wa kwenda shule.

Pia kuna haja ya kudhibiti wimbi la vijana kukimbilia mijini, kwa kuwaandalia mazingira mazuri vijijini, badala ya kuishia kufanya biashara ndogo ambazo mwisho wa siku haziwezi kuwainua kiuchumi.

Nguvukazi ya vijana kwenye sekta ya kilimo ni muhimu kwa maendeleo ya taifa, hasa kwa kuzingatia kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo wa taifa, hivyo mazingira rafiki kwa vijana wapende kilimo ni muhimu.

Kwanza kabisa, si vibaya kuhakikisha ardhi inayofaa kwa kilimo inapatikana na kutengwa katika halmashauri zote nchini kwa ajili ya vijana ambao wako tayari kufanya uwekezaji katika kilimo.

Vilevile ni muhimu vijana wakawezeshwa kifedha na pia kuhakikisha wanapata pembejeo, zana za kilimo na huduma nyingine wanazohitaji kwa ajili ya shughuli zao, ziwe zinapatikana wa bila usumbufu.

Jambo jingine ni uwezeshwaji wa kifedha, kuweka miundombinu ya matumizi ya umwagiliaji kwa ajili yao lakini zaidi wawe na uhakika wa masoko ya bidhaa za kilimo ili wawe na uhakika wa mazao yao.

Watoto wenye umri wa kwenda shule na vijana wakubwa wanaokimbilia mijini kufanya biashara, ni vyema kila kundi lidhibitiwa kwa utaratibu wake kwa ajili ya kusaidia kuyaweka kwenye mstari.

HABARI KITAIFA

# RC Chalamila awataka Mwanza kunywa pombe

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Albert Chalamila, amewataka wakazi wa mkoa huo kunywa pombe kwa kuwa inachangia kukuza uchumi wa nchi kupitia kodi za serikali.

Chalamila ameyasema hayo jana jijini Mwanza alipozungumza na uongozi wa Mamlaka ya Mapato (TRA).

Alisema watu wakiacha kunywa pombe maana yake mapato ya serikali yatapungua kwa sababu unywaji pombe unaongeza kodi za serikali.

Kuhusu baadhi ya baa kupiga kelele za muziki, Chalamila alisema hapo ndiyo mahala pake, kwa kuwa asingetegemee sehemu kama hizo ziwe na utulivu


Aidha, alitaka TRA kukusanya mapato ya serikali kwa ''kuwafinya kidogo'' wafanyabiashara wasiotaka kulipa kwa hiari.

Alisema licha ya Rais Samia Suluhu Hassan kuagiza TRA kutumia busara na akili, lakini wakati mwingine lazima wawe wakali kwa wafanyabiashara wasiotaka kulipa kwa hiari.

Kuhusu wafanyabiashara kutoa risiti halali wanapouza bidhaa zao, Chalamila alitaka TRA kusimamia hilo.

Aidha, Chalamila alisema wafanyabiashara wengi hawatoi risiti za mashine wakati wa kuuza bidhaa zao, hatua ambayo inaikosesha mapato serikali na kuagiza TRA kuweka mkazo katika eneo hilo.

Mkuu wa huyo wa mkoa baada ya kukabidhiwa ofisi, alianza ziara ya kutembelea taasisi mbalimbali za serikali na kuzungumza na watumishi.




Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho (katikati), akikabidhiwa mfano wa hundi ya Sh. milioni tano kutoka kwa Meneja wa Biashara wa Benki ya CRDB, Nickson Mushi (kulia), wadhamini wa mkutano wa mashauriano na wadau wa sekta ya ujenzi kwa mwaka 2021 ulioandaliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) jijini Dar es Salaam jana. Wa (pili kulia) ni Msajili wa CRB, Rhoben Nkori na (wapili kushoto) ni Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Consolata Ngimbwa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Majaliwa afunguka kuhusu ujambazi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUFUATIA wimbi la matukio ya ujambazi hivi karibuni, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka Watanzania kutoa taarifa za viashiria vya matukio hayo ili vyombo vya dola vifanye kazi inayokusudiwa.

Majaliwa alitoa kauli hiyo bungeni jana katika kipindi cha maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Makete (CCM), Festo Sanga.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema kwa siku za karibuni nchini kumekuwa na wimbi la ujambazi likiendelea hasa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Mbeya na Arusha.

"Kitu ambacho kilikuwa kinahatarisha usalama kwa wafanyabiashara wetu, mali za vijana na usalama wa nchi yetu, je, ipi kauli na maelekezo ya serikali dhidi ya vitendo viovu inavyoendelea kwenye Taifa letu?" Alihoji.

Majaliwa akitoa majibu bungeni, aliwaambia wabunge kuwa serikali inao wajibu wa kulinda raia wake, usalama wao, mali zao lakini kuhakikisha kwamba wanaendesha shughuli zao za kila siku kwa amani na utulivu.

"Kazi hii nzuri inafanywa vizuri na vyombo vyetu vya dola, lakini kazi hii mara kadhaa tumewaomba Watanzania tushiriki kwenye ulinzi wa nchi yetu pale kila Mtanzania anapotakiwa kupaswa kulinda, kujilinda yeye mwenyewe na jamii inayomzunguka na hatimaye jamii kwa ujumla." "Ili kujiridhisha na usalama wa nchi unakuwa imara, Jeshi letu la Polisi linafanya kazi nzuri sana na siku mbili, tatu hizi tulisikia kazi nzuri waliyoifanya jijini Dar es Salaam na Watanzania wote walisikia na wameona kazi ambayo wameifanya ya kudhibiti hao majambazi," alisema.

Aliwahakikishia wabunge kuwa serikali inaendelea na kazi hiyo ya kuwahakikishia wananchi usalama wa raia na mali zao.

"Watanzania wote wanajua hata Mheshimiwa Rais kupitia moja ya hotuba zake kitaifa ameweza kuwaonya wale wote wanaofikiria kwamba huu ni wakati wa kufanya maovu nchini na amewataka wale wanaofikiria kufanya hivyo waache mara moja."

"Anapoagiza haya maana yake anaagiza vyombo vya ulinzi na usalama kuchukua hatua kali dhidi ya wale wote ambao wanasababisha madhara ya usalama kwa Watanzania," alisema.

Alisema jukumu lao ni kuhakikisha kuwa Watanzania wanashiriki kwenye ulinzi wa nchi na kila Mtanzania pale anapohisi au anapoona kuna dalili za upotevu wa amani ni vyema kutoa taarifa kwenye vyombo vya sheria ili hatua kali zichukuliwe.

"Kwa hiyo bado tunaendelea na jukumu la kulinda nchi la kulinda watu wake na mali zao na usalama wao ili nchi hii iendelee kuwa na tunu yake ya amani wakati wote," alisema.

# Wachimbaji tanzanite wafa kwa kukosa hewa

**Na Jaliwason Jasson,** SIMANJIRO

WACHIMBAJI wadogo wawili wa madini ya tanzanite yaliyopo Mirerani, Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, wamepoteza maisha, baada ya kukosa hewa wakiwa ndani ya mgodi wa 'Mulla'.

Watu hao wanadaiwa kwenda kutafuta madini hayo katika mgodi huo, ambao haufanyi kazi kwa muda mrefu.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi, Marison Mwakyoma, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa wachimbaji hao walikutwa wamefariki Mei 26, mwaka huu, majira ya saa 5:00 asubuhi.

"Inasemekana kwamba wachimbaji hao waliingia kwenye mgodi huo wa Kampuni ya Kilimanjaro Mining, unaomilikiwa na mfanyabiashara wa Jiji la Arusha, Alhakim Mulla.

"Chanzo cha vifo hivyo ni wachimbaji hao kuingia kwenye mgodi huo ambao haufanyi kazi, wakakosa hewa na kufariki dunia." Alisema Kamanda Mwakyoma.

Mwakyoma, aliwataja waliofariki ni Omary Shabani (44), Mkazi wa Kazamoyo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani na Frank Ndekirwa (43), ambaye ni Mkazi wa Tengeru, mkoani Arusha.

Kwa mujibu wa Kamanda Mwakyoma, Polisi inaendelea na uchunguzi wa tukio hilo, kwa kushirikiana na maofisa wa madini ili kubaini matukio mengine juu ya ajali hiyo.

Mmoja wa wachimbaji walioshuhudia tukio hilo, Elias Lazaro, alisema watu hao waliingia kwenye mgodi huo, wakidhani kuwa watapata madini ya tanzanite.

Badala yake, wachimbaji hao walikosa hewa kutokana na mgodi huo kuondolewa mashine ya oxgen, baada ya kusimamisha kazi ya uchimbaji wa madini.

Mei 7, mwaka huu, wachimbaji wengine wawili wamefariki dunia na watatu kujeruhiwa, baada ya kutokea mlipuko wa baruti kwenye mgodi wa madini ya tanzanite wa Kampuni ya California Camp uliopo Mirerani.

Watu hao walilipukiwa na baruti hiyo, walipokuwa katika kitalu B (Opec) kwenye mgodi unaomilikiwa na Deo Minja (48), mkazi wa Njiro jijini Arusha.

## Wapinga watoto kupewa chanjo minyoo, kichocho

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAZAZI na walezi wa wanafunzi wa Shule ya Msingi Mhungula 'B', Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wameugomea uongozi wa shule kuwachanja chanjo za minyoo na kichocho watoto wao, wakidai ni za virusi vya corona.

Hayo yalijitokeza jana katika kikao cha wazazi na uongozi wa shule hiyo baada ya ajenda ya utoaji wa chanjo za minyoo na kichocho kuwasilishwa na uongozi wa shule kwa wananchi na kuibuka kwa malumbano ya kuzikataa chanjo hizo, wakidai ni za virusi vya corona.

Mmoja wa wazazi, Gizibarth Mahewa, alidai chanjo hizo kwa sasa hawazihitaji, na kwamba ni mbinu inayotumika kuhadaa wananchi kuwaruhusu watoto wao kuchanjwa chanjo ya corona.

"Tumekuwa tukiona kwenye maeneo mengi duniani namna ambavyo chanjo ya corona inasababisha madhara makubwa kwa wananchi ambao wamechanjwa, hofu yetu kwa watoto wetu ni kuchanjwa chanjo hiyo," alidai Mahewa.

Naye Salum Bundala, alisema, kwa sasa wananchi wamehamaki sana, kutokana na uwapo wa janga la corona na kukosekana kwa uhakika wa chanjo ya ugonjwa huo.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Believe Joseph, aliwataka wazazi hao kuachana na mambo yanayosambazwa kwenye mitandao ya kijamii, badala yake wazingatie maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya juu ya chanjo ya corona.

Pia alivitaka vyombo vya habari na wataalamu wa afya kuendelea kutoa elimu zaidi juu ya chanjo hiyo ili kuwaondoa hofu wananchi na kuwaruhusu watoto wao kupata chanjo mbalimbali zinazotolewa shuleni.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Mhungula, Nestory Lugomola, alisema ili kuondoa hofu hiyo kwa wananchi, wamejipanga kuanza kutoa elimu ya chanjo kupitia majukwaa ya mikutano ya uongozi wa serikali ya mtaa, na atahakikisha watoto wa wananchi wanapata chanjo hiyo.

# Mama adai kubakwa na kundi la vijana tisa

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

KATIKA hali isiyo ya kawaida mama mwenye miaka 41 (jina linahifadhiwa), anadai kufanyiwa unyama wa kubakwa na vijana tisa wanaodaiwa kuwa ni jamii ya Kimasai katika kijiji cha Mtakuja, Kata ya Dakawa, wilayani Mvomero.

Amedai kuwa licha ya baadhi ya vijana hao kukamatwa na polisi, wanaonekana mitaani wakiranda na yeye kutishiwa maisha.

Akisimulia mkasa huo, alisema Aprili 13, mwaka huu, alikuwa na mume wake wakitoka dukani kufuata mahitaji majira ya saa moja usiku na kuvamiwa na kundi hilo la vijana.

Alisema walipovamiwa walianza kumshambulia mume wake kwa fimbo na marungu, licha ya kujaribu kujitetea walizidiwa nguvu na kumgeukia yeye na kuanza kumfanyia unyama huo.

"Walinifanyia unyama huo kwa kupokezana," alisema.

Alisema wakati wakiendelea na unyama huo, walikuwa wakiwapigia simu wenzao waje kujiunga kumfanyia unyama huo bila ya kujali kama baadhi yao anawafahamu.

"Walipomaliza kufanya kitendo chao pale uwanjani walipigia simu mwenzao ambaye namfahamu naye akaja wakanitoa uwanjani wakanipeleka karibu na kijijini kuna kaburi, wakarudia kufanya kitendo kile, nilipojaribu kutaja jina la kijana ninayemfahau wakataka kunichoma na kisu, lakini huyo kijana akawazuia," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Albinus Mgonya, ambaye alipata taarifa za tukio hilo, alitaka kupata maelezo ya hatua zilizochukuliwa kutoka kwa Mkuu wa Polisi Wilaya ya Mvomero, Sospeter Kungura, ambaye alisema awali walikuwa wanawashikilia watuhumiwa watatu na kati yao wawili waliachiliwa kwa dhamana na mtuhumiwa moja bado anashikiliwa na jeshi hilo.

Alisema mpaka sasa hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwamo kufikisha jalada kwa Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Morogoro, kwa ajili ya kumfikisha mtuhumiwa mahakamani wakati uchunguzi ukiendelea.

"Tayari jalada lilishapelekwa ofisi ya mashtaka mkoa na limesharudi, lakini huwa tunakabiliwa na changamoto ya kukosa ushirikiano kwa waathirika ndio maana lawama zote zinarudi kwa Jeshi la Polisi," alisema Kungura.

Hata hivyo, Mkuu wa Wilaya alionesha kutoridhishwa na hatua zilizochukuliwa na kulitaka jeshi hilo wilayani humo kuwakamata watuhumiwa wote tisa waliopo mtaani. Alisema haiwezekani tukio hilo litokee tangu Aprili 13 na jeshi hilo linazungusha upelelezi wa kesi hiyo wakati taarifa za wahusika zinajulikana huku wengine wakiendelea kuonekana mtaani.

"Kitendo hiki kama serikali hatuwezi kukivumilia hata kidogo OCD na timu yako nataka ndani ya siku 30 watuhumiwa wote wawe wameshakamatwa na uniletee ofisini kwangu taarifa ya kukamatwa kwao kwasababu watu wanajulikana kwa majina, lakini kesi haiendelei na mama wa watu anaendelea kuteseka," alisema Mgonya.



Mfanyabiashara wa Kariakoo, Adelard Lyakurwa (katikati), akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam jana kusikiliza mashtaka yanayomkabili ya kutishia kuua kwa bastola. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kesi madai mfanyabiashara kutishia kuua kunguruma Juni 8

**Na Kulwa Mzee**

KESI ya kutishia kuua kwa bastola inayomkabili mfanyabiashara wa Kariakoo, Adelard Lyakurwa (58), inatarajia kuanza kusikilizwa Juni 8, mwaka huu.

Lyakurwa alifika katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala jana na kusomewa maelezo ya awali dhidi ya mashtaka yake mbele ya Hakimu Mfawidhi, Martha Mpaze.

Wakili wa Serikali, Nancy Mshumbusi, alidai mshtakiwa anashtakiwa kwa kumtishia kuua kwa bastola mfanyabiashara maarufu Valence Lekule.

Mshtakiwa anadaiwa kutenda kosa hilo kinyume na kifungu cha 89 (2)(a) cha sheria ya kanuni ya adhabu sura ya 16, iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

Wakili Nancy alidai Julai 30, mwaka huu maeneo ya Kariakoo, Mtaa wa Mbaruku na Swahili, Wilaya ya Ilala akiwa na lengo la kuua, alimtishia Valence Lekule kumuua kwa kutumia bastola huku akijua kufanya hivyo ni kosa la kisheria.

Mshtakiwa anadaiwa kuwa ni mkazi wa Msasani na siku ya tukio alikamatwa na kupelekwa Kituo cha Polisi cha Kati kwa tuhuma za kutishia kuua.

Mshtakiwa alikana maelezo yote kuhusu tuhuma zake, lakini alikiri kwamba tarehe iliyotajwa alikuwa maeneo ya Kariakoo, Mtaa wa Mbaruku na Swahili na Mei 12, mwaka huu, alikamatwa na kufikishwa mahakamani.

Baada ya kudai hayo upande wa Jamhuri ulidai unatarajia kuita mashahidi saba katika kesi hiyo na kuomba ipangwe tarehe ya kuanza kusikilizwa.

Hakimu Mpaze aliahirisha kesi hiyo na kupanga kuanza kusikilizwa Juni 8, mwaka huu na kuamuru upande wa Jamhuri walete mashahidi wawili siku iliyopangwa.

Wakili wa Utetezi, Richard Mbuli, alipokea maelezo ya mlalamikaji kwa ajili ya kufanya maandalizi ya kesi hiyo.

Mshtakiwa yuko nje kwa dhamana yenye masharti ya kuwa na wadhamini wawili waliokuwa na barua zinazotambulika kisheria na walisaini dhamana ya maandishi ya shilingi milioni moja.

HABARI KITAIFA

# Wadau bidhaa za viungo wanolewa

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

WAZALISHAJI, wauzaji, wasambazaji na wadau wengine wa bidhaa za viungo mkoani Morogoro wamepatiwa mafunzo kuhusu uzalishaji bidhaa zenye ubora na viwango vinavyokubali ili kupanua soko lao ndani na nje ya nchi. Mafunzo hayo yanalenga kuwawezesha kuondokana na uuzaji, usambazaji na uzalishaji wa viungo kwa nia ya kujikimu, bali wafanye biashara zenye tija na hatimaye waweze kushiriki katika uchangiaji wa pato la Taifa.

Hayo yalisemwa juzi Matombo mkoani Morogoro na Meneja Mafunzo na Utafiti wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Hamis Sudi Mwanasala, wakati wa mafunzo yaliyotolewa kwa wauzaji, wasambazaji, wazalishaji na wadau wa viungo ili wabadilike na kuondokana na uendeshaji wa shughuli zao kwa nia ya kujikimu.

Aliwataja wadau hao kuwa ni wauzaji, wasambazaji na wazalishaji wa viungo ikiwamo iriki, mdarasini, karafuu na vinginevyo, kutokana na mkoa huo kuwa na wazalisha na wadau wengi wanaojipatia kipato kupitia bidhaa za viungo.

Mwanasala alisema; "Serikali baada ya kutambua kwamba wajasiriamali wana mchango mkubwa sana katika kukuza uchumi wa nchi hii, wanasisitizwa wabadilike kuzalisha kwa wingi bidhaa zenye ubora ambazo zitaingia kwenye soko ndani na nje ya nchi bila vikwazo vya kibiashara." Alisema shirika hilo linawataka wafuate viwango, lakini pia kanuni bora za afya na mazingira. Kupitia mafunzo haya pia alisema maofisa wa shirika hilo waliwapatia washiriki elimu juu ya usajili wa majengo ya bidhaa za vyakula na vipodozi.

Aliongeza kuwa awali majukumu ya usajili majengo ya bidhaa za vyakula na vipodozi yalikuwa yakitekelezwa na iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA), lakini kwa sasa yanafanywa na TBS.

Baadhi ya wadau walioshiriki mafunzo hayo ni SIDO na Tantrade. Kwa upande wa Tantrade walitoa elimu kuhusiana na masuala ya masoko hususan masoko ya nje ya vyakula, kutokana na bidhaa za viungo kuhitajika sana huko.

Kwa upande wa SIDO walitoa elimu kuhusu uchakataji na uzalishaji bora wa vyakula.



Mafundi wakiandaa msingi kwa ajili ya ujenzi wa sekondari ya Kijiji cha Bwai Kumsoma, Kata ya Kiriba, wilayani Musoma, mkoani Mara, mwishoni mwa wiki, ambayo baada ya kukamilika kutaifanya kata hiyo kuwa na sekondari mbili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kamati yaipa mapendekezo Ardhi

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, imetoa mapendekezo katika maeneo kadhaa ili kuongeza ufanisi wa Wiraza ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuwahudumia wananchi. Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Aloyce Kwezi, aliyataja maeneo hayo bungeni wakati akiwasilisha maoni ya kuwa ni mwenendo wa upatikanaji wa fedha zinazotengwa na kueleza kuwa kuna changamoto kubwa ya ucheleweshaji wa fedha kutoka Hazina jambo lililochangia udhaifu katika utekelezaji wa mipango mingi.

La pili, ufanisi wa wizara katika kukusanya maduhuli, kuwa ni muhimu halmashauri zikachochewa kukusanya kodi, hiyo kwa kuelimisha umma umuhimu wa pango la ardhi kwa wakati, na kukamilisha kuingiza wateja wote kwenye mfumo wa kielektroniki.

La tatu, ufanisi wa mfumo wa kupanga, kwamba ni umuhimu fedha zikatolewa kutekeleza miradi ya maendeleo na kwamba serikali itoe fedha kwa wakati.

La nne, kupima na kumilikisha ardhi, alisema kamati imebaini kuwa mfumo wa kukopesha halmashauri fedha kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi una changamoto.

Kwezi alisema mapendekezo ya kamati ni kuongeza idadi ya halmashauri zinazopaswa kukopeshwa kutoka 24 hadi 50 kwa mwaka, kujenga bajeti za kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi ya vijiji sita kwa mwaka.

La tano, ufanisi wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Ardhi kwa kuhakikisha inajulikana kwa umma na kuitaka serikali kuhusisha muundo wake na kuwa na mfuko wa upangaji ardhi, kuwa na bajeti na kuongeza wafanyakazi.

# Viongozi Afrika wapewa somo kuikabili Covid-19

**Na Enock Charles**

RAIS Paul Kagame ameshauri viongozi wa Afrika kuchukua hatua za pamoja kukabiliana na athari za virusi vya Corona katika bara hilo ili kujikomboa na janga hilo lililoikumba dunia kuliko kila nchi kupambana kivyake.

Akizungumza katika siku ya UBA Afrika katika mjadala ulioletwa na Benki ya UBA ukihusisha viongozi wa Afrika kuhusu athari za Covid 19, Rais Kagame alisema imeathiri nchi nyingi za Kiafrika kiuchumi kutokana na kufungwa kwa mipaka na kwa hivyo aliwataka viongozi wengine wa Kiafrika wajiunge pamoja na kujadili njia sahihi za kujikwamua kiuchumi.

"Athari za Covid 19 zimeathiri serikali na sekta binafsi, tunapaswa kujifunza kutokana na janga hili na kuwekeza zaidi bajeti yetu katika mfumo wetu wa kitaifa wa afya. Hili sio janga la mwisho kutoka kwa ulimwengu na inatupasa sisi kama Afrika kujiweka tayari na kujiandaa na majanga mengine yanayoweza kuja kutokea hapo kwa baadae alisema Kagame

"Nadhani ni muhimu kwa viongozi wa Afrika kuja pamoja na kujadili athari za janga hili kwa pamoja kama viongozi, tunaweza kujadili juu ya sababu za migogoro ya hili au lile, nadhani kuheshimiana ndio njia bora ya uhusiano kati ya Afrika na ulimwengu wote, tunazungumza juu ya matatizo lukuki kwenye Bara letu la Afrika, njaa na umasikini, lakini huu sio utambulisho wetu .

Mwenyekiti UBA Group na Mwanzilishi wa Taasisi ya Tony Elumelu Foundation, Tony Elumelu, alisema Benki ya UBA ilianzisha siku hiyo kisha kuanzisha mazungumzo ya Siku ya Afrika ya UBA na kwa mwaka huu ilikuwa ni awamu ya tatu, na kwamba benki hiyo hukaribisha viongozi wa Afrika wanaolijua na kutambua vizuri bara hilo hasa kwenye maeneo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Viongozi walioalikwa mwaka huu ni Ngozi Okonjo-Iweala, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Biashara Ulimwenguni (WTO), Dk. Tedros Adhanom Ghebreyesus, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), Rais Kagame na Makhtar Sop Diop, Mkurugenzi Mkuu, Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC) ambapo kwa kuzingatia changamoto za sasa za COVID 19 imechukua hatua zaidi za usalama kwa kufanya mazungumzo hayo kwa njia ya mtandao.

Mkurugenzi wa Shirika la Afya Ulimwenguni Dk. Tedros Adhanom Ghebreyesus alisema WHO inafanya kazi siku kwa siku kuleta suluhisho la haraka kwa usambazaji wa vipimo na chanjo vya Covid, na kwamba ni muhimu kwa bara hilo kuondokana na utegemezi wa chanjo kutoka nje ya bara hilo.

Ngozi Okonjo-Iweala, Mkurugenzi Mkuu wa WTO, alitaka nchi za Afrika kusamehewa madeni na kupata nafuu huku akiunga mkono hoja ya nchi za Afrika kutengeneza chanjo yake na kuachana na utegemezi kutoka Ulaya na Marekani.

# Spika aiagiza wizara kuandaa majibu upya swali la mbunge

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameagiza Wizara ya Madini kuandaa majibu upya ya swali la Mbunge wa Ndanda (CCM), Cecil Mwambe, kwa maelezo kuwa halijajibiwa.

Akitoa agizo hilo jana bungeni baada ya Naibu Waziri, Prof. Shukurani Manya, kujibu swali la Mbunge huyo aliyehoji mpango wa serikali baada ya kukamilika kwa mradi wa utafiti wa madini ya Graphite kata ya Chiwata.

Spika Ndugai alisema: "Ndio maana huwa nawaambia tusome swali na tuangalie majibu, sidhani kama Mheshimiwa Mwambe una haja ya kuuliza swali la nyongeza kwa sababu swali hili halijajibiwa Profesa, narudisha tena swali hili Wizara ya Madini nitalipangia tarehe nyingine, mtatakiwa kujibu swali hili, tujibu maswali waheshimiwa Mawaziri, swali ni rahisi tu serikali ina mpango gani, sasa mmepiga maneno wee jibu halipo."

Katika majibu ya Wizara hiyo katika swali la Mwambe, Prof. Manya alisema mikoa ya kusini mwa Tanzania ikiwamo Lindi na Mtwara imebarikiwa hazina kubwa ya madini ya kinywe ambayo ni madini ya kimkakati yanayohitajika kwa kiasi kikubwa kwa sasa duniani kutokana na matumizi yake kama malighafi za viwandani.

Alisema kutokana na uwapo wa hazina ya madini hayo, zipo kampuni nyingi zinazomiliki leseni za utafutaji na uchimbaji madini ya kinywe katika maeneo mbalimbali nchini ikiwamo mikoa ya Lindi na Mtwara.

"Hadi sasa kwa nchi nzima kuna jumla ya leseni 68 za utafutaji, leseni 24 za uchimbaji wa kati na leseni moja ya uchimbaji mkubwa wa madini ya kinywe," alisema.

Aidha, alisema katika Kata ya Chiwata ambayo ipo Jimbo la Ndanda, wilayani Masasi kuna leseni mbili za uchimbaji wa kati zilizotolewa kwa Kampuni ya Volt Graphite Tanzania Limited tarehe 18/10/2018 baada ya kukamilisha shughuli za utafiti.

"Kinachosubiriwa ni Kampuni hiyo kuanza uchimbaji na uchakataji wa madini ya kinywe katika leseni hizo," alisema.

Alisema mpango wa serikali ni kuona kampuni zinazomiliki leseni za utafutaji madini zinakamilisha shughuli za utafiti na kuomba leseni za uchimbaji mkubwa au kati.

"Uwapo wa leseni hizo utapelekea kuanzishwa kwa miradi ya uchimbaji ambayo italeta mapinduzi makubwa ya kiuchumi katika Sekta ya Madini," alisema.

Aidha, alisema uanzishwaji wa miradi hiyo utaiwezesha serikali kukusanya mapato zaidi, kutoa fursa za ajira kwa Watanzania hasa wanaoishi katika maeneo yanayozunguka miradi, uhaulishaji wa teknolojia, fedha za kigeni na manufaa mengine kwa jamii kupitia local content na CSR.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (wa pili kushoto), Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (kushoto) na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dk. Festo Dugange, Bungeni, jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**




**Habari zote Na Augusta Njoji, DODOMA**

## 'Mikakati ya Polisi sasa inajitosheleza kuukabili ubakaji'

SERIKALI imesema kwa sasa mikakati ya Jeshi la Polisi inatosheleza kukabiliana na tatizo la ubakaji na ulawiti, hivyo haihitaji kuanzisha kikosi maalum kwa kuwa makosa hayo ni jinai na yana adhabu kisheria.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Angelina Malembeka.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema jeshi hilo lina uwezo wa kukomesha tatizo sugu la ubakaji na ulawiti kwa watoto wadogo nchini.

"Je, ni kwanini serikali isiunde kikosi maalumu cha kuwashughulikia watu wanaojihusisha na vitendo vya ubakaji na ulawiti?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Chilo alisema katika kupambana na tatizo sugu la ubakaji na ulawiti Jeshi la Polisi limejiwekea mikakati thabiti inayohusisha kufuatilia vyanzo vya makosa na kuyatafutia ufumbuzi.

"Moja ya mikakati hiyo ni kutoa elimu kwa kushirikisha jamii kupitia madawati ya unyanyasaji wa jinsia yaliyopo kwenye vituo vyote vikuu vya polisi, aidha hutoa elimu ya mapambano dhidi ya makosa ya aina hii katika shule za msingi na sekondari, maadhimisho ya kitaifa na matamasha mbalimbali,"alisema.

Aidha, alisema wale wote wanaobainika kutenda makosa hayo huchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Hata hivyo, alisema kwa sasa mikakakati ya jeshi la polisi inatosheleza kukabiliana na tatizo hilo bila kuhitaji kuanzisha kikosi maalum kwani yote ya jinai ikiwamo ya udhalilishaji yana adhabu kisheria.

"Makosa haya yanatendeka miongoni mwa jamii hivyo ni lazima jamii nzima ishirikiane kuyapinga na kuyakataa kwa kutoa taarifa vituo vya polisi na kwenda kutoa ushahidi mahakamani ili adhabu stahiki zitolewe kwa wahalifu,"alisema.

# Serikali yajiweka kando mikopo kwa wanaume

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema kwa sasa haikusudii kuanzisha mpango wa kuwawezesha mikopo wanaume.

Naibu Waziri TAMISEMI, Dk. Festo Dugange, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Moshi Mjini (CCM), Priscus Tarimo.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji nini mpango wa serikali kuwawezesha kina baba nao kiuchumi baada ya mpango wa Halmashauri kuwawezesha kinamama, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kuwa na mafanikio makubwa.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange alisema Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kutoa mikopo isiyo na riba kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

"Mikopo hiyo hutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 kifungu cha 37A inayoelekeza kutenga asilimia 10 ya mapato yanayokusanywa na Halmashauri kwa ajili ya mikopo ya asilimia 4 kwa wanawake, asilimia 4 kwa vijana na asilimia 2 kwa watu wenye ulemavu," alisema.

Alisema lengo la mikopo hiyo ni kusaidia makundi maalum katika jamii ambayo hayawezi kupata mikopo katika Mabenki ya Biashara na Taasisi za Fedha kwa sababu ya masharti magumu ikiwamo dhamana na riba kubwa.

"Hivyo, Serikali ilitoa kipaumbele kwa makundi ya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu kwa kuwa wengi wao hawakopesheki katika mabenki na taasisi za fedha. Kwa sasa Serikali haikusudii kuanzisha mpango wa kuwawezesha wanaume/akinababa,"alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alihoji serikali kama ipo tayari kuongeza umri kwa kundi la vijana kufikia miaka 45 ili wanaume wanufaike na mikopo hiyo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema kundi la vijana hasa wa kiume wamekuwa wakinufaika na mikopo hiyo na ni wale wenye umri wa miaka 18-35 na serikali haijaweka mpango wa kuongeza umri kwa kuwa lengo la mikopo hiyo ni vijana.




Ukurasa 13

Wimbo wa Ajira ‘Bongo’ umepoteza mrindimo

# BUFE

IJUMAA MEI 28, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 12

**Mfano aina yake, vijana vijijini wasukwa kitaalamu wakitumia soko kwao kujiajiri**

MJUE ALIVYOVUKA

# Ndani miaka 10, akitoka maskini mwenye Sh. 5,000, leo Sh. bil 2.3

**New York, Marekani**

AKIWA akiwa na 24, hakuwa na chochote kabisa. Akaunti yake benki ilikuwa na Dola za Maekani 2.26 (Sh. 5198) pekee na hakuwa na kazi. Wakati huo ndipo alipoamua kurejea nyumbani kwa wazazi wake.

“Nilikuwa nalala kwenye kitanda kile kile nilichokuwa nakilalia nikiwa mdogo,” Grant Sabatier, mwandishi wa kitabu cha Financial Freedom, kinachouzwa kwa wingi nchini Marekani.

Pia, ndiye mwanzilishi wa tovuti maarufu ya Millennial Money, anasema alipokuwa nyumbani, alijifunza namna ya kuendesha matangazo hayo kupitia mafunzo na miongozo iliyokuwa inapatikana katika tovuti na ndipo akaanza kutafuta kazi.

“Mara ya kwanza nilipotuma maombi kutafuta kazi hiyo ya uuzaji kupitia njia ya digitali, nikaipata,” anasimulia.

Kuanzia hapo, anajivunia maisha kubadilika kwenye nyumba ya wazazi wake na akajiwekea lengo la kuweka akiba na kuwekeza kadri ya uwezo wake.

Katika kipindi cha miaka mitano, anasema alijikuta kuwa na akiba ya Dola milioni 1.25.

“Nilikuwa naishi kwenye nyumba duni, gari yangu ilikuwa mbaya na muda wangu mwingi nilikuwa nautumia kufanya kazi na kuweka akiba,” anasimulia Sabatier.

**ALIPATAJE PESA?**

Muda wake wa ziada, alikuwa anaendesha kampeni zake za kibiashara mitandaoni akiwa na wateja kadhaa.

“Wakati fulani nilikuwa na vyanzo 13 tofauti vya kujipatia kipato,”



Grant Sabatier. **PICHA: MTANDAO**

ansimulia kwamba, baada ya mwaka mmoja alianzisha kampuni yake ya kuendesha matangazo kwa njia ya digitali na miezi sita baadaye, akaanzisha kampuni ya pili.

“Nilistaafu nikiwa na miaka 30,” anasema na kuendelea: “Niliweka pesa nyingi kiasi kwamba nikaamua kustaafu nikiwa na miaka 30 na leo hii kazi ninayofanya ni kuandika kwenye blogu.”

Sabatier, mwenye umri wao miaka 34 sasa, anaendeleza simulizi: “Nilistaafu kufanya kazi katika kampuni kwa sababu sihitaji tena pesa, naweza kuishi kwa kutumia pesa ambazo nimetengeneza katika kipindi changu chote cha maisha kilichosalia.”

Anasema, kustaafu hakumaanishi kuwa mtu hawezi kufanya tena kazi, bali ni kufanya unachokipenda.

Sabatier anasimulia, kufanya kazi yenye uhusiano na biashara mtandaoni haikuwa kile anachotaka maishani, lakini alichukulia kazi hiyo kama njia moja ya kumpa kipato.

“Kuanzia mwanzo lengo langu lilikuwa kupata pesa za kununua uhuru wangu. Nilikuwa na shauku ya kupata pesa,” anasema.

Na mwisho wake dhamira iliyokuwapo ni kuweka akiba na kuwekeza akiwa bado na umri mdogo.

“Nilinunua uhuru wangu. Ilinichukua miaka mitano, miezi mitatu na siku sita,” anasema kwamba, msingi wa kufikia lengo hilo ulitokana na sababu, akizitaja:

“Kuna bahati ndani yake, kufanya kazi kwa bidii, kuwa na shauku na kuwekeza ulichoweka akiba kwa njia nzuri.”

Sebastian anasema kwamba alihifadhi asilimia 82 ya mapato yake na alianza kuwekeza mwaka 2010, wakati soko lilipokuwa halifanyi vizuri na kupata faida kupitia alichopata katika njia zake zingine za uwekezaji.

“Nilifanikiwa kuweka asilimia 82 ya kipato changu. Bado naona uwekaji akiba kama fursa wala sio kujinyima,” aliongeza.

Sabatier anasema kwamba, kuna hatua tatu kufikia uhuru wa kifedha, akiziorodhesha ya kwanza kuwa ni kadiri unavyoendelea kuweka akiba, ndivyo unavyoweza kufikia uhuru wa kifedha kwa haraka.

“Ikiwa utaweka akiba ya asilimia tano itazaa 10, hautawahi kufikia uhuru huu. Kiwango muafaka ni kuweka akiba ya asilimia 50.

“Lakini kwa hilo kutokea, utalazimika kuishi katika nyumba ndogo pamoja na wengine kwa kipindi cha takriba miaka mtano,” anasema kwamba aliwekeza katika soko la hisa Pili, anataja kutumia fursa zote anazopata kutafuta pesa. Akitoa mfanil kuanza na kazi za kuajariwa, lakini my anafuta vyanzo vingine vya kipato kando na mashahara.

Tatu, anasema ni kuwekeza akiba, mbayo yake binfasi anataja ni katika kuwekeza katika majengo na soko la hisa.

“Kadiri unavyowekeza, utakuwa unapunguza muda wako unaotumia kutafuta pesa,” anasema.

Kwa hivi sasa, Sabatier anaishi na mke wake mjini New York na licha ya kwamba, ni moja ya miji ya gharama ki maisha nchini Marekani,

Anaeleza mengi anayopenda kufanya huwa ni bure kama vile kusikiliza muziki na marafiki au kutazama filamu na mke wake.

Anahitimisha kuwa: “Kadiri unavyoendelea kufanya matumizi ndivyo utakavyolazimika kufanya kazi kwa miaka mingi.” Wa sasa ana akiba ya Dola za Mrerkani milioni moja au Sh. bilioni 2.3.

- ***Kwa mujibu wa BBC.***

UCHUMI

# Mfano aina yake, vijana vijijini wasukwa kitaalamu wakitumia soko kwao kujiajiri

## •Washika tenda na kuwa maarufu kila mahali

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**



TANZANIA ni nchi yenye mfumo wa elimu watoto wote wanaanza masomo kwa shule za awali na idadi inapungua kadri wanavyosonga mbele katika ngazi tofauti, hususan shule za sekondari.

Sheria nchini inatamka elimu ya msingi inaishia darasa la saba. Ni haki ya kila mtoto anayefaulu kuendelea na sekondari na wasiofaulu wanarejea kwenye mbadala kuyaanza maisha au njia nyingine za elimu mbadala kama vile za ufundi

Mchujo wa safari baada ya shule za msingi, sekondari hadi kidato cha nne, wanaovuka hufika hadi kidato cha sita, ambako nako wanaofaulu hujiunga na elimu ya juu vyuoni.

Ni ukweli ndani ya mfumo huo, kuna idadi kubwa ya vijana wanaohitimu masomo katika ngazi mbalimbali, hubakia mitaani bila ajira au njia mbadala wa kuwaingizia kipato.

**NGAZI ZA AJIRA**

Wakati vijana hao wakibaki mitaani bila ajira au kazi rasmi, jamii wanayoishi inakabiliwa na changamoto kuwezesha vijana wajiajiri na hata kujihalalishia maisha.

Kero zao kuu zinajumuisha ukosefu wa vyoo bora, kukithiri taka mitaani, kukosa nishati ya uhakika kutumiwa na jamii, pia kuendesha mitambo yao.

Aidha, ndio inayoliibua shirika lisilo la kiserikali la CRS, lilipoanzisha mradi wa kuwasaidia vijana wapate ujuzi unaowawezesha wajiajiri, kwa kufanya kazi kwenye jamii katika makazi yao.

Mradi huo ulianza kwa majaribio katika Halmashauri za Mbeya, Chunya na Mbarali, ukishirikisha vijana 120 waliopewa mafunzo ya ujasiriamali, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na ufundi uashi.

Mhandisi Mshauri wa CRS, Godfrey Mpangala, anasema ni mafunzo yanayolenga kuwaboresha vijana kupitia mazingira na kuangalia kero za usafi wake, katika mazingira yanayoshindwa kutatuliwa kwenye jamii.

Anasema, wazo la kuanzishwa mradi huo ni kuwawezesha vijana kuwasaidia kutumia fursa zinazopatikana kwenye maeneo yao, ikijumuisha biashara, kero zilizopo kijamii na kuzifanyia utatuzi unaowanufasisha kimapato.

> **“Suala la kuwekeza rasilimali fedha kwa ajili ya usafi wa mazingira vijijini, linawekezana kwa sababu serikali imeunga mkono jitihada hizo, kwa kuwapatia vijana mkopo ambao uliwawezesha kununua vifaa vya ujenzi au kuendesha shughuli zao kupitia biashara ya ujenzi wa vyoo bora aliongeza,” anasema Mhandisi Mpangala.**

Ndivyo ilivyo miradi ya ujenzi ya vijana chini ya CRS wilayani Chunya, Mbeya katika hatua tofauti.
**PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Anasema utafiti wao ulibaini kuwajibikia usafi wa mazingira kama uzoaji taka na majitaka, ukiwa umewekezwa zaidi mjini kuliko vijijini, hivyo wakabaini zinahitajika vijijini, ambako hali ya kiafya hairidhishi.

Mpangala anasema waliamua kusaidia upatikanaji wa huduma za usafi wa mazingira vijijini, kwa kuwapa mafunzo vijana wa maeneo hayo, ili watumie kuhamasisha au kutoa huduma hizo moja kwa moja kwenye jamii zao.

Anasema, waliwapeleka baadhi ya vijana katika Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) jijini Mbeya, wakapate ujuzi ambao watakapotumia kufanikisha azma yao.

Inatajwa wanufaika hao wako 121 kutoka wilaya za Chunya, Mbarali na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, walikopatiwa mafunzo VETA kwa mwezi mmoja, ikigharimiwa na CRS na wakatunukiwa vyeti katika fani za ufundi ujenzi, ujasiriamali, usafi wa mazingira na TEHAMA, iliyowawezesha kukuza na kutafuta masoko kupitia simu zao za mkononi.

Anasema vijana hao walianza kuhamasisha ujenzi wa vyoo bora na usafi wa mazingira, huku wenyewe wakiwa ndio mafundi wa kujenga vyoo bora.

**BAADA YA MAFUNZO**

Mpangala anaeleza, baada ya hapo walitumia ujuzi wao kujenga vyoo bora vya kisasa kwenye shule tisa za mfano, ndani ya wilaya za mradi kwa kuzingatia mwongozo wa serikali.

“Tuliwajengea uwezo wa kufanya biashara ya ujenzi wa vyoo bora kwa kipindi cha miaka mitatu tangu kuanzishwa kwa mradi wa usafi wa mazingira, tukilenga maeneo ya vijijini.

“Tumefanikiwa kuwahamasisha wananchi kujenga vyoo bora ili kukabiliana na magonjwa ya milipuko, pia kukuza uchumi wao kwa kutumia ujuzi wao.

“Suala la kuwekeza rasilimali fedha kwa ajili ya usafi wa mazingira vijijini, linawekezana kwa sababu serikali imeunga mkono jitihada hizo, kwa kuwapatia vijana mkopo ambao uliwawezesha kununua vifaa vya ujenzi au kuendesha shughuli zao kupitia biashara ya ujenzi wa vyoo bora aliongeza,” anasema Mhandisi Mpangala.

Aidha, anaueleza kuwa ni mradi waliouanzisha kwa vikundi, ili kupata mitaji ya kuendesha biashara ya kujenga vyoo wakinunua vifaa na mengine ya ujasiriamali.

Mpangala anasema, mradi umefanikiwa kwa zaidi ya asilimia 90, vijana hao sasa wanaweza kujenga nyumba, kuboresha mirefeji, kujenga shule na kushiriki miradi mingine binafsi na kiserikali.



Anasema imetimu miaka miwili sasa halmashauri wanakoishi vijana ziliwapatia mikopo ya kuwawezesha kiuchumi ya Sh. milioni 44 na wamesharejesha kwa asilimia 90.

**KUTOKA KWA WAFADHILI**

Meneja Mradi wa asasi, Human Development Innovation Fund (HDIF), Eveline Nguma, anasema waliamua kufadhili Mradi wa Usafi wa Mazingira, baada ya kuiona jamii, ina mwamko mdogo katika matumizi ya vyoo bora.

Anasema imetimu miaka mitatu sasa, mabadiliko yameanza kuonekana vijana hao wakijenga vyoo kwa gharama nafuu kwao wanakoishi.

Nguma anasema, mradi huo ulianzishwa mwaka 2018 na umeshawapatia vijana ajira, kuisaidia jamii kutumia vyoo bora, kujenga mifumo ya baiogesi ya kutumiwa majumbani, kupitia biashara ya ujenzi wa vyoo inayotangazwa kwa simu kuwafikia wateja wa maeneo mbalimbali.

“Ni mradi mzuri uliowezesha vijana kujipatia ajira kupitia ujuzi walioupata, wengi waliishia kupata elimu ya darasa la saba na wengine wachache walikuwa na elimu ya kidato cha nne.

“Kwa sasa, wote wanajiona kama vile wanaelimu ya kutosha kutokana na ujuzi walio nao kuwasaidia kujiajiri na kujipatia riziki bila shida,” anasema.

Anasema biashara ya ujenzi inafanyika kwa msimu na kupitia mitaji walio nayo, waliamua kujishughulisha na biashara nyinginezo kupitia uwezeshaji wa serikali.

**MKUU WILAYA**

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Wiliam Ntinika anazishauri wilaya zote za mkoa Mbeya, kutumia asilimia 10 ya bajeti ya halmashauri kuviwezesha vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu wazielekeza kwa vijana hao wajuzio wa ujenzi.

Ntinika anazishauri halmashauri zitoe kipaumbele kwa vijana hao 121, huku akifafanua: “Vijana hawa wapewe mikopo ya vifaa vya ujenzi ili wafanye kazi zao bila vikwazo vyovyote, tuendelee kuwahamasisha waliopata ujuzi huo wajiunge kwenye vikundi ili wanufaike na ninawataka maofisa maendeleo wa Halmashauri zetu wawatambue.”

Ofisa Afya wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Christopher Mathias, anasema kuanzia mwaka 2018 hadi 2021, jumla ya vyoo 234 vimejengwa katika halmashauri hiyo, ikiwamo Kata za Maendeleo, Igoma na Tembela.

**MFANO WA MAFANIKIO**


Miongoni mwa vijana walionufaika na mradi, ni Zawadi Melele kutoka Kata ya Tembela, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, anakiri mradi umembadilishia mtaji na kuendesha ujasiriamali kwa kiwango cha juu.

Zao lake, amemudu ujenzi wa vyoo na fedha za kujenga nyumba ya kisasa pamoja na kuhudumia familia, pasipo matatizo.

“Nilihitimu kidato cha nne lakini matokeo hayakuwa mazuri. Nikawa mkulima ambaye sina mtaji, nilikuwa nafanya vibarua bado sikuwa na uhakika na maisha. Nilipobahatika kuchaguliwa na CRS kuwa miongoni mwa wanufaika nilipata mafunzo ya ufundi VETA,” anasema Melele.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Wimbo wa Ajira ‘Bongo’ umepoteza mrindimo






**NA JOSEPH KULANGWA**

NI dhahiri shayiri kwamba kuna wengi nchini tunadanganyana sana. Ni vyema sasa tukapunguza kuwa mbali na ukweli, kwa sababu hatuwezi kamwe kukomesha hilo kwa hulka tuliyo nayo wengi wetu.

Bado hatuko sawa katika ukweli kuhusiana na ajira kwa vijana wetu. Tumekuwa siku zote tukiimba kutengeneza ajira kwa vijana kama msingi wa kuwaletea maendeleo, pia kuiletea maendeleo Taifa hili tajiri.

Lakini, kadri siku zinavyosonga mbele, ndivyo vijana wanazidi kuhitimu masomo yao vyuoni na kuingia mitaani bila ajira, huku tukiendelea kuwahimiza na kuwashawishi kujiajiri, bila kuwapo upana wa hoja mitaji itakapopatikana.

Ni hivi siku za karibuni, tamko kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu inayoshughulikia Vijana, Ajira, Kazi na Wenye Ulemavu, ikishirikiana na Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), ilitangaza kuwaita vijana 12,625, ili iwapeleke katika vyuo vyake 68 nchini wakapate mafunzo ya fani mbalimbali.

Vijana 40,292 walijitokeza kuchukua fomu katika chuo kimoja tu cha Chang’ombe, Dar es Salaam na waliorudisha fomu hizo ni zaidi ya 19,000. Hao ni wale waliopata taarifa ya kuwapo tangazo hilo.

Pia, hao ni walio karibu na vyuo husika. Fikiria ambao hawakupata taarifa, fikiria wale waliopata taarifa, lakini wakawa mbali na vyuo, wakawa hawana nauli za kuwafikisha huko, achilia mbali pesa ya kuwakimu kula na kulala.

Waliotakiwa ni 12,000 na waombaji 40,000, tena katika chuo kimoja kati ya 68. Hapo tatizo lipo bila ya kupepesa macho. Bado mchujo ukishapita, wapo watakaorudi mitaani kusubiri bahati nyingine ya mtende.

Lakini, katika mchujo huo, tusijeshangaa wanaochukuliwa ni watokao katika familia ambazo walau zinajimudu kimaisha, huku walalahoi wakirejea ‘kupiga lapa’ mitaani, ‘wakichakura’ kutafuta ajira.

Haitoshangaza ikitokea watakaopata kuwa wenye ‘vimemo’ kutoka kwa wazazi wenye mamlaka tena wametafutwa na wazazi, hata kama hawataki kusoma kozi hizo.

Juzikati hapa, Spika Job Ndugai akasikika akiziagiza kamati za kufuatilia mchakato wa ajira zinazotolewa na serikali, kuhakikisha kunakuwapo uwazi na haki katika kuajiri vijana. Hivi wahusika walimsikia Spika?

Aliungwa mkono na Mbunge wa Muleba Kaskazini, Charles Mwijage, yule aliyepata kuchachamalia ujenzi wa viwanda nchini, akisema taarifa za ajira nchini kuna wakati zinakosa uhalisia, kwamba zinatangazwa, lakini zikifuatiliwa hakuna kitu.

Hajatoka nje ya ukweli, kwa sababu kuna shirika moja kubwa tu hapa nchini (nalihifadhi leo tu), limekuwa likisababisha maumivu ya kichwa kwa baadhi ya watu.

Shida ni kwamba linatangaza nafasi za ajira, wakati wenye sifa ingawa walalahoi wanapokanyagana kuomba, tayari kuna wenzao walishaitwa na kuanza mafunzo.

Yaani, unaambiwa tangazo limetoka leo na mwisho pengine ni katikati ya mwezi, wenzako walishajua nafasi hizo kitambo na walishaitwa kuanza mafunzo. Wewe unapoomba, wao wameshaanza ajira. Ni Kazi kweli kweli! Huko ndiko kudanganyana.

Labda, siku moja ifanyike sensa kama iliyofanyika enzi zile za Rais John Magufuli, kwa wasiokuwa na vyeti, kwamba vikusanywe vyeti vya kuzaliwa vya vijana wanaoajiriwa, tuone kama hatutakuta idara au shirika fulani lina ndugu watupu, kwa sababu tu wanatoka familia za watu wa nasaba fulani kiuchumi.

Unasoma na mtu mathalan ‘mburura’ kabisa darasani, mnamaliza shule pamoja, mnahitimu chuo pamoja, mwenzio anafeli, lakini siku mbili tatu ana ajira, anakuringishia wewe uliyejidai ‘kipanga’, uko unazurura mitaani kutafuta ajira. Ukiuliza shida nini, unapata jibu ni mtoto wa mlalahai.


Inashindikanaje kwa watoto wa walalahoi, vipanga lakini wanakosa ajira kwa hila kufikiria kushuka Kusini mwa Tanzania na kuvuka mpaka? Inashindikanaje wa aina hii kuapa bora kufa kuliko kuteseka na elimu kichwani isiyomfaidisha?

Tusidanganyane kuwa eti bora kupata elimu kuliko ajira! Nani aliishi kwa kula elimu, nani alikula bila ajira? Nani atajiajiri bila mtaji? Kama tunataka usawa tusiwashike mikono watoto wa walalahai na kuwapiga mateke wa walalahoi! Alamsiki!

BIASHARA

# Naibu Waziri Ulega azuru sekta Uvuvi na kuwapa njia za kuibuka

## • Ushirika, sheria nyavu, mikopo...
## • Ataja anavyolenga kuisuka upya



Wavuvi wa wilayani Sengerema katika Ziwa Victoria, walipokuwa kazini.

**Na Yasmin Protace**

SERIKALI imekuwa ikipambana na wavuvi watumiao nyavu zisizo na sifa katika kazi hiyo, maarufu 'nyavu haramu' jambo linalofahamika vyema kwa jumuiya na sekta hiyo ya kiuchumi.

Katika hilo, wamekuwa wakichangia hata samaki kuvuliwa wakiwa wadogo na kuharibu mayai ya samaki. Kwa ujumla, wanaharibu mazalia ya samaki na daima kutokuwa endelevu.

Uvuvi wa nyavu hizo haramu, zinachangia kuwarudisha nyuma wavuvi kwa jumla, pia kuvuliwa samaki walio chini ya kiwango stahiki.

Hivyo, serikali imekuwa ikiendelea kupambana na aina ya uvuvi huo haramu, kwa kuweka taratibu za kuwatambua na hatua mbalimbali za upatikanaji nyavu za uvuvi, tangu utengenezaji wake, hadi inavyosambazwa kumfikia mvuvi husika.

**NAIBU WAZIRI AZURU**

Ni hatua ya kudhibiti kusambaa nyavu zisizohitajika kisheria nchini. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, anasema

baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Kanyala wilayani Sengerema, Mwanza alipokuwa ziarani kikazi akitaka suala la kuchoma nyavu ama lipungue au liishe kabisa.

"Tumejipanga vyema sana wavuvi. Mmekuwa mkipata sintofahamu kubwa, unaenda dukani kununua nyavu ya milimita nane, ukija nayo huku ikipimwa inaonekana iko chini ya milimita hizo.

Ni kinyume na sheria na wewe kuchukuliwa hatua, sasa tutapambana na wauzaji na wasambazaji wa nyavu hizo," anasema Ulega.

Angalizo lake ni katika kuhakikisha nyavu za uvuvi zinakuwa na viwango vinavyotambulika, akiahidi wizara husika itaweka utaratibu wa kuwapo kipimo kimoja kitakachotambuliwa kitaifa.

**VIGEZO VYA TBS**

Kwa mujibu wa Waziri Naibu Ulega, wizara kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), itafikia hatua hiyo, ikiwa ni namna ya kumwokoa mvuvi asiendelee kuumizwa, kwa kuarifiwa kuwa nyavu zake ziko kinyume na sheria.

Pia anawapongeza wakazi wa Kijiji cha Kanyala, kwa kuonyesha mwamko wakishirikiana na serikali kuepuka zana haramu, ambazo pia ni kinyume na sheria za nchi.

**USHIRIKA WAVUVI**

Kuhusu uanzishwaji kwa vyama vya ushirika vya wavuvi, Ulega anasema serikali hivi sasa imepanga kuwawezesha wavuvi kupitia vyama hivyo, kwa kuwapatia mikopo ya kuwawezesha kununua vyombo vya kisasa vya shughuli za uvuvi.

"Vikundi vya ushirika vinafanya vizuri sana na wengine wamejitengenezea vyombo vya uvuvi. Tuweke utaratibu mzuri. Tusirudi nyuma, nimekuja kutazama namna navyosonga mbele. Nataka kurudisha ari ya kufanya vizuri sana, nataka nirudi tena hapa kukabidhi hundi." anafafanua Ulega.

Azma yake naibu waziri, anataka vyama vya ushirika vya wavuvi vinufaike na mikopo, kupitia taasisi mbalimbali, ikiwamo Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

Vivyo hivyo, anasema vyama vya ushirika ambavyo vimekwishapatiwa mikopo, kujitahidi katika busara ya kufanya marejesho kwa wakati, ili viendeleze sifa za kukopesheka kwenye taasisi za fedha, vivyo hivyo kuwezesha vyama vingine vya uvuvi kupata mikopo.

**VIONGOZI SERIKALI**

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Emmanuel Kipole, anakemea vitendo vya rushwa na kuwataka wavuvi wasikubali kutoa rushwa kwa mtendaji yeyote wa serikali, kwani kufanya hivyo ni kuhalalisha kuendelea kuwapo vitendo hivyo vya kutumia nyavu haramu.

Anasema, watendaji wanaohusika na ukamataji wa zana za uvuvi zisizotakiwa kisheria, kwani wanasaidia kuondoa magumu katika uvuvi.

Wakazi wa Kijiji cha Kanyala, wanamtaka Naibu Waziri Ulega, kwamba baadhi ya vyama vya ushirika vya wavuvi vinakosa mikopo kutoka taasisi mbalimbali za kifedha, licha ya kufuata taratibu stahiki.

Kwa mujibu wa Ulega, alishafanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, aliyeahidi kufanyia kazi rai ya kuwasaidia mikopo wavuvi.

Wakazi hao wameiomba serikali kutokomeza nyavu haramu za sehemu hiyo, kwani wamekuwa wakipata hasara kwa kununua nyavu zisizotakiwa kisheria, bila ya kufahamu na wanaishia kukamatwa na nyavu zao zinazochomwa moto, hali inayowarudisha nyuma kimaendeleo.

**USHIRIKA WAVUVI**

Akiwa wilayani Sengerema, Naibu Waziri Ulega aliyeambatana na Mkuu wa Wilaya, Emmanuel Kipole na Mbunge Shigongo, walifika katika kijiji cha Zilagula akakutana na Chama cha Ushirika wa Wavuvi Zigalula, walikoshuhudia namna wanavyotumia mkopo wa shilingi milioni 100.7 kutoka TADB.

Hapo walikagua namna wanavyotumia fedha za mkopo kutengeneza boti za uvuvi, vichanja vya kuanikia dagaa, kujenga eneo la kuhifadhi samaki.

Pia, ugebui huo wa viongozi walijulishwa mikakati mbalimbali ya chama hicho cha ushirika inafanya kupitia fedha hizo.

Naibu Waziri alipozungumza na wanakijiji, wa Zilagula, anakitaka Chama cha Ushirika wa Wavuvi Zilagula kuwasaidia vijana na akawataka wataalamu kufikishwa kijijini,

ili kutoa elimu ya matumizi bora ya fedha za mikopo, iwe na tija zaidi kwa jamii husika.

Ulega anakitaka chama hicho kufanya kazi vizuri zaidi, likiinuke kimaendeleo kama vile kuweza kununua boti za kisasa zaidi za uvuvi na wanakijiji wa Zilagula kuunga mkono Ushirika wa Wavuvi Zilagula.

Anafafanua kuwa kupitia chama hicho, wavuvi wataweza kuuza samaki kwa bei nzuri zaidi, badala ya kulanguliwa na watu wachache, wanaofika kununua kwa jumla, lakini kwa bei ndogo huku wakienda kuuza kwa bei kubwa katika masoko mengine ya mbali.



Nyavu haramu, zinazopigwa vita zikiwa zimekamatwa wilayani Sengerema. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



# Mkakati waja kukidhi mahitaji soko la ajira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema mwaka huu inatarajia kufanya utafiti utakaosaidia kuboresha elimu ya ufundi ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira na ujuzi nchini.

Utafiti huo ni pamoja na kuangalia hali ya nguvu kazi iliyopo kama wanaajirika katika soko la ajira na hali ya rasilimali watu iliyopo nchini na ujuzi wao.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Vijana, Kazi, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kongamano la wadau wa elimu ya ufundi lililoandaliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF).

Alisema mwaka huu serikali imeamua kufanya utafiti huo utakaoleta tija katika elimu ya ufundi na pia kuwa na takwimu za nguvu kazi na ujuzi ulipo nchini.

"Huu utafiti tunalenga kuangalia hali ya nguvu kazi tuliyo nayo na tunaamini itasaidia kujua ni asilimia ngapi ya vijana wetu wanaweza kuajirika katika soko la ajira tulionao."

"Sekta zipi zina, fursa zipi zaidi kwenye soko la ajira ili kufundisha ufundi unaoendana na mahitaji yaliyopo kwa taifa tusipofanya utafiti huo tutashindwa kuendelea mbele," alisema.

Aidha, alisema katika kuangalia hali ya rasilimali watu iliyopo nchini na ujuzi wao, itasaidia kufahamu Watanzania waliopo ndani na nje ya nchi wanafananaje na mahitaji yaliyopo kwasasa.

"Wizara yangu tunashughulikia vibali vya wageni, tumeanza kukusanya takwimu kwanini wawekezaji wanataka kuleta wataalamu wakati Watanzania wana viwango hivyo, itasaidia kujua ni maeneo gani ambayo hatuna ujuzi ili kusaidia katika kupanga mipango ya mafunzo hapa nchini tutakuwa tumefanya jambo kubwa litakaloendana na mahitaji ya kiuchumi ya taifa letu," alisema.

Kadhalika, aliwahamasisha wadau wa sekta binafsi kufungua vyuo vingi vya sayansi na teknolojia ili kusaidia kuwa na nguvu kazi yenye ufundi wa kutosheleza mahitaji nchini na kueleza vikwazo ambavyo serikali itaviondoa ili kufanikisha hilo.

"Pia mweleze kama kuna vikwazo ambavyo tutaviondoa ili mfanikiwe kufungua vyuo vingi, kwanini tuna vyuo 92 tu kati ya 184? Tujue tunafanya nini ili kulingana na mahitaji ya sasa."

"Sisi serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan tumekubaliana tunataka kutumia sekta binafsi kuwa sehemu ya uchumi wa nchi, hatuwezi kujenga vyuo vyote ni muhimu sekta binafsi kusaidia ili kuzalisha nguvu kazi itakayotumika kwenye miradi yetu ya kimkakati," alisema.

Mhagama alisema serikali itakuwa tayari kupokea ushauri utakaotolewa kupitia kongamano hilo ili kuyafanyia kazi.

Alisema kongamano hilo limewakutanisha wataalamu waliobobea kwenye elimu ya mafunzo ya ufundi na serikali inaamini litasaidia kutathmini ubobezi uliopo na mazingira ya sasa.

"Kongamano hili mliamua kuliandaa kwa ushirikiano kati ya NACTE na TPSF, nawapongeza kwa kuwakutanisha hapa na TPSF ndio mwajiri anayebeba watu wanaozalishwa kwenye ufundi," alisema.

Alisema kongamano hilo litaonesha namna ambavyo imeweza kuchangia uchumi wa Tanzania.

"Ulimwenguni kote elimu ya mafunzo ya ufundi yanamchango mkubwa kwenye uchumi, tutumie kongamano letu kutafakari kwa kiasi gani kila mmoja kwenye eneo lake ametumia elimu ya ufundi kama kichocheo endelevu cha ukuaji wa uchumi," alisema.

Alifafanua kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita Tanzania imeingia kwenye uchumi wa kati kabla ya muda uliopangwa.

"Sisi ni wadau muhimu katika miradi ya kimkakati ikiwamo wa bomba la mafuta, Kongamano hili liwe ni sehemu ya kurudisha mtazamo na ushirikiano wetu wa pamoja," alisema.




Mwenyekiti wa Chama cha Sekta ya Ulinzi Binafsi Tanzania (TSIA) Taifa, Felix Kagisa, akizungumza na wajumbe wa mkutano mkuu wa uchaguzi uliofanyika jijini Dodoma jana, baada ya kuchaguliwa tena kukiongoza chama hicho kwa kipindi cha miaka mitano. Kulia ni Mwenyekiti wa TSIA Kanda ya Kati, Lukanus Kayombo, Makamu Mwenyekiti wa TSIA Taifa, Eliuta Mwanjawike (wa pili kulia) na (kushoto) ni Mhazini Mkuu, Kara Remtullal. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mfumo kufuatilia taarifa za wajawazito

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kuja na mfumo wa ufuatiliaji wa taarifa za wajawazito wote kuanzia wanapofika kliniki kwa mara ya kwanza hadi baada ya siku 42 za kujifungua.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wataalamu wa afya katika kikao kazi cha maandalizi ya utengenezaji wa mfumo huo.

Alisema anataka kuwapo na ufuatiliaji wa taarifa za wajawazito ili kujua wangapi wanaopata huduma za afya.

"Nataka muwe mnafuatilia taarifa za wajawazito na kujua maendeleo yao kuanzia wanapofika kituoni siku ya kwanza mpaka baada ya kujifungua kwa data za kila siku na kujua kwa namna gani wajawazito au mama baada ya kujifungua ameweza kupata huduma zetu na muweze kuchukua hatua pale mnapoona changamoto," alisema.

Aidha, Waziri Gwajima alisema ili kuwa na mfumo wenye ufanisi lazima kuwapo na matumizi sahihi ya takwimu huku akiwataka wataalamu wa afya katika kazi zao kuhakikisha wanachukua takwimu zote zinazohitajika kwa ajili ya matumizi katika mfumo huo.

"Serikali katika kupambana na vifo vya wajawazito imefanya mambo mengi ikiwamo kuanzisha kampeni maalum ya jiongeze tuwavushe salama iliyoanzishwa na aliyekuwa Makamu wa Rais na sasa ni Rais Samia Suluhu Hassan, yenye lengo la kupunguza na kudhibiti vifo vitokanavyo na uzazi," alisema. Alibainisha kuwa serikali imejenga vituo vingi vya huduma ngazi zote na mwamko wa wajawazito wanaojitokeza kuhudhuria kliniki umekuwa mkubwa.

"Lakini bado elimu inahitajika kutolewa kwa wajawazito ili wafike katika vituo vya kutolea huduma za afya na kuanza kliniki mapema, sasa hivi mwitikio umeongezeka wajawazito wanajitokeza na kujifungua katika vituo vya kutolea huduma kati yao wengine wanafariki lakini tunajitahidi wakati alipokuwa kliniki tunagundua hatukumfuatilia vizuri hiki ndio kitu tunachoimarisha ili ufuatiliaji uwe imara," alisema.

## Shirika lawawezesha wananchi lishe bora

**Na Mwandishi Wetu,** CHAMWINO

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Save The Children kupitia mradi wake wa lishe endelevu, limeanza kutoa elimu na kuwawezesha wananchi mifugo ambayo itasaidia kupata lishe bora katika familia ili kusaidia kupambana na utapiamlo na udumavu kwa watoto.

Mradi huo unaotekelezwa na Shirika hilo kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID) ambapo wananchi wanawezeshwa mtaji wa ufugaji wa wanyama wadogowadogo wenye virutubisho ambavyo vitasaidia katika ukuaji wa mtoto na kuwafundisha kilimo mchanganyiko kwa makundi ya vyakula.

Akizungumza katika uzinduzi wa mradi huo kijiji cha Chinangali I, Wilaya ya Chamwino, Meneja Mradi wa Lishe Endelevu wa shirika hilo, Gedion Muganda, alisema wamegawa sungura, vifaranga wa samaki na vifaranga vya kuku.

"Kupitia mradi huu tunataka kuziwezesha familia kuwa na lishe bora kwa kugawa vifaranga wa kuku, samaki na sungura tunaamini nyama hii inavirutubisho vingi ambavyo vitawezesha watoto kukua kwa afya."

"Tunagawa kwa wananchi wachache kama mtaji ambapo wakizaliana wanawapa mbegu wananchi wengine hivyo tunaamini baada ya mwaka uzao utakuwa mkubwa na kila mwananchi atakuwa na uwezo wa kupata lishe bora na kipato kupitia wanyama hao," alisema.

Alisema kupitia mradi huo wamepanga kupunguza tatizo la udumavu kwa watoto chini ya miaka tano, kuongeza idadi ya wanawake walio katika umri wa kuzaa kula vyakula vyenye mchanganyiko kwa kiwango kinachokubalika.

Muganda alisema kupitia mradi huo utawafikia wanawake 92,572 walio katika umri wa kuzaa, watoto 75,118 walio chini ya miaka tano na vijana walio katika rika balehe.

Alitaja kazi zitakazofanywa kupitia mradi huo ni kuwajengea uwezo watoa huduma za afya kwenye ngazi ya kliniki ili kutoa huduma bora za lishe na ushauri nasaha, kutoa mafunzo ya mkoba wa siku 1000 kwa wahudumu wa afya na kutoa mafunzo kwa wanawake vinara zaidi ya 30 kutoka kwenye kata mbalimbali katika mikoa nne.

Akizindua mradi huo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Vumilia Nyamoga, aliwataka wataalamu wa mifugo wa halmashauri kuhakikisha mradi huo unafanikiwa kwa kiwango cha juu ili kuzikomboa kaya zenye lishe duni.

"Nitoe maelekezo kwa wataalamu wa mifugo wa halmashauri kuhakikisha kwamba mradi huu unafanikiwa, kila mmoja katika eneo lake apange ratiba maalumu ya kuwatembelea wanufaika wa mradi huu ili kuwapatia ushauri wa kitaalamu na ushauri uwe kwa maandishi," alisema.





# Kijana matatani madai kuua baba kwa panga

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linamshikilia kijana, Daniel Manga maarufu kwa jina la 'Hofu', mkazi wa Kijiji cha Iheha wilayani Mbarali kwa tuhuma za kumuua baba yake, Victor Manga (79), kwa kumcharanga mapanga.

Jershi la Polisi limesema mtuhumiwa kabla ya kufanya kitendo hicho, alimtuhumu baba yake kuwa ni mchawi.

Akizungumza na wandishi wa Habari jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema mtuhumiwa alikamatwa na Jeshi hilo Mei 25, mwaka huu kufuatia msako uliofanywa na askari kwa kushirikiana na wananchi.

Alisema mtuhumiwa alimcharanga baba yake na panga kichwani na kwenye mkono wa kulia, hali iliyosababisha kuvuja damu nyingi na kupoteza maisha.

"Baada ya tukio hilo, Jeshi la Polisi lilifanya msako katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Mbarali na kumkuta mtuhumiwa akiwa amejificha kwenye Kijiji hicho, na ndipo wakamkamata na kumfikisha kituoni," alisema Kamanda Matei.

Alisema Jeshi hilo linaendelea na msako katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo ili kuwabaini watu wote wanaojichukulia sheria mkononi ili wachukuliwe hatua za kisheria.

Aliwataka wananchi kuachana na imani potofu zinazowafanya wawe wanajichukulia sheria mkononi ikiwemo kuamini uchawi akisisitiza kuwa Jeshi hilo litaendelea kuwachukulia hatua kali.

Matei aliwataka wananchi kusuluhisha migogoro ya kifamilia nay a kijamii kwa kutumia vyombo vya sheria badala ya kutumia njia ya kujichukulia sheria mkononi akidai kuwa ni kosa kwa mujibu wa sheria.

Aidha, aliwataka wananchi pia kuendelea kutoa taarifa kwa jeshi hilo ama kwa viongozi wa Serikali wanapobaini ugomvi wa wanafamilia ili hatua zichukuliwe mapema za kudhibiti ugomvi huo kabla haujaleta madhara zaidi.

Katika hatua nyingine, Kamanda Matei alisema Jeshi hilo linawashikilia watu sita wanaohusika na mtandao wa wizi wa pikipiki na bajaji mkoani humo pamoja na uvunjaji wa nyumba za wananchi na kuiba vitu mbalimbali.

Kamanda Matei aliwataja waliokamatwa kuwa ni Samson Daniel (47) mkazi wa Uyole jijini Mbeya, Samwel Isack (49), mkazi wa Jiji la Mwanza na Mtumigwa Moses (23), mkazi Wilaya ya Kyela.

Wengine ni Christantus Eugin (26) na Fauz Said (20), wakazi wa jijini Dar es Salaam pamoja na Steven Chamshama (32), mkazi wa Block T jijini Mbeya.

Alisema watuhumiwa walihojiwa na kukiri kushiriki matukio mbalimbali ya wizi katika mikoa ya Mbeya, Katavi, Kigoma na Mwanza.

"Lakini huyu Chamshama alipopekuliwa alikutwa na vidonge 40 vinavyotumika kuwalewesha waendesha pikipiki kisha kupora pikipiki hizo, upelelezi unaendelea na ukikamilika wahusika watafikishwa mahakamani," alisema Kamanda Matei.

Vilevile Kamanda Matei alisema Jeshi hilo linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za kukutwa na dawa za kulevya aina ya bangi zenye uzito wa gramu 535.

Aliwataja watuhumiwa hao ni Nicholous Mbonde (24) mkazi wa Forest jijini Mbeya, Isaka Philipo (25) mkazi wa Tarafani katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi na Kened Francis (21), mkazi wa Chapakazi Mbalizi.



Baadhi ya vibarua katika shamba la miti la Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kiwira, mkoani Mbeya, wakiendelea na shughuli ya kujaza udongo kwenye vitalu kwa ajili ya kupanda miche ya miti, juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Maelfu ya wakulima kushiriki maonyesho

**Na Grace Mwakalinga ,**

MBEYA.

ZAIDI ya wakulima 2,000 kutoka maeneo mbalimbali nchini wanatarajiwa kushiriki kwenye maonyesho ya kilimo biashara ambayo yameandaliwa na serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI).

Taasisi hiyo imeanda maonyesho hayo kwa kushirikiana na wadau wengine wa kilimo, yatakayofanyika leo jijini Mbeya.

Maandalizi ya maonyesho ya kilimo biashara ambayo mwaka huu yanafanyika jijini Mbeya kwa mara ya tatu mfululizo, yamekamilika na sasa wakulima wanahamasishwa kufika ili wapate elimu na teknolojia za kilimo bora cha kibiashara.

Akizungumza jana na wanahabari kuhusu maandalizi hayo, Kaimu Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha TARI- Uyole, Leonard Sabula, alisema wamejiandaa kutoa teknolojia za aina mbalimbali kwa wakulima ili waweze kuzalisha kwa tija.

Alisema wakulima na wafanyabiashara kutoka maeneo mbalimbali nchini wanatarajiwa kushiriki kujifunza na kuongeza mnyororo wa thamani kwenye mazao wanayozalisha.

"Taasisi na mashirika mbalimbali yakiwamo kampuni ya usambazaji pembejeo za kilimo yanashiriki maonyesho hayo yenye lengo la kuwasaidia wakulima kujifunza mbinu za uzalishaji kwa kutumia teknolojia za kisasa, lakini pia kuunganishwa na masoko licha ya maonyesho haya TARI, Kituo cha Uyole wameendelea kuwapatia wakulima elimu ya kilimo bora pamoja na kuwasambazia miche ya aina mbalimbali," alisema Sabula.

Prudence Gerald, mwakilishi wa Baraza la Nafaka Afrika Mashariki, alisema maonyesho hayo yamekuwa na tija kwa wakulima kwani wengi waliopata elimu wameongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao tao.

Ipyana Mwakasaka, mwakilishi wa AGRA, alisema wamejiandaa kuwapatia wakulima elimu ya kuongeza thamani ya mazao ili kukidhi mahitaji ya soko la dunia.

# DC: Fanyeni biashara kwa uhuru, kulipa kodi mapema

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, amewataka wafanyabiashara wa mkoa huo kufanya biashara zao kwa uhuru na kulipa kodi kwa wakati kwa sababu Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), imekaribisha mazungumzo kwa wale wenye madeni kuyalipa kwa awamu.

Aliyasema hayo juzi jijini Mbeya kwa niaba ya Mkuu wa mkoa huo, Juma Homera, wakati akifungua kikao cha mazungumzo kati ya TRA na Chemba ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA) kilichofanyika katika Ukumbi wa Mkapa jijini Mbeya.

Ntinika aliwataka wafanyabiashara kutumia wakati huo kufanya mazungumzo na TRA ili waingie mikataba ya namna ya kulipa madeni yao ya kodi kwa wakati kwa maelezo kuwa Serikali ina nia njema ya kuwainua wafanyabiashara.

"Serikali, kupitia Rais Samia Suluhu Hassan, imewakaribia wafanyabiashara kwa kuweka mazingira mazuri ya kufanyia biashara na kuwaachia wafanyabiashara wafanye biashara zao kwa uhuru lakini hapo hapo mtambue wajibu wa kulipa kodi kwa hiari," alisema Ntinika.

Pia aliwataka wafanyabiashara hao kutumia fursa hiyo kushirikiana na TRA kutatua matatizo ya kikodi yanayowakabili ili kulipa kodi kwa mujibu wa sheria.

Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo, alisema TRA itaendelea kuweka mazingira rafiki ya ulipaji kodi ikiwamo la kuanzisha mifumo ya kieletroniki inayowezesha wafanyabishara kuzilipa kwa urahisi.

"Tutaendelea kutoa elimu ya kodi kwa wafanyabishara kupitia kampeni ya mlango kwa mlango inayoendelea mikoa mbalimbali na tunasisitiza zaidi matumizi ya mashine za EFD na mifumo mingine ya kieletroniki ya ulipaji kodi ila kurahisisha maisha ya wafanyabiashara katika dhana nzima ya kulipa kodi kwa wakati," alisema Kayombo.

Kayombo alisema mikutano kama hiyo ya kukutana na wafanyabiashara itafanyika katika mikoa 19 ya Tanzania bara ili kuimarisha uhusiano wao na wadau hao.

Makamu Mwenyekiti wa TCCIA, Dk. Kulwa Meshack, aliwataka wafanyabiashara na wanachama washiriki mikutano hiyo kwa sababu ni jukwaa zuri la kutatua matatizo yao na kuimarisha uhusiano na TRA.



# SUK yaleta ufumbuzi changamoto za kisiasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema uundaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), umeleta ufumbuzi wa changamoto za kisiasa zilizokuwa zikiikabili Zanzibar.

Alisema hatua hiyo imelenga kuwawezesha wananchi kuishi kwa amani na utulivu na kuharakisha kasi ya kupata maendeleo.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu Jijini Zanzibar, alipozungumza na Uongozi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Alisema serikali inakusudia kuweka nguvu zaidi kuyapatia ufumbuzi matatizo mbalimbali ya wananchi yanayowasilishwa kwake, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi alizozitoa wakati wa kampeni ya uchaguzi mkuu wa 2020. Pia, alisema serikali itashirikiana Tume hiyo kufanikisha vyema majukumu yake na kutimiza matakwa ya kikatiba.

Alipongeza juhudi za Tume hiyo kuweka mfumo mzuri wa mawasiliano ya kimtandao na kuwafikia wananchi wengi zaidi, akibainisha ukubwa wa Tanzania.

Dk. Mwinyi alisema tayari serikali imeshalipatia ufumbuzi suala la kuwapo uwiano wa nafasi za ajira kati ya vijana wa Tanzania Bara na Zanzibar kupitia vikao vya kamati ya masuala la Muungano, hivi sasa Zanzibar itapata wastani wa asilimia 21 ya nafasi hizo.

Aliahidi kulipatia ufumbuzi tatizo la ofisi linazoikabili Tume hiyo Unguja na Pemba ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Naye, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Tanzania, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu, alisema tangu Rais Dk. Mwinyi alipochaguliwa kuiongoza Zanzibar amethibitisha nia ya dhati ya kuwaunganisha Wazanzibari, baada ya kushirikiana na Chama cha ACT-Wazalendo na kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Alisema kupitia busara zake na kwa kushirikiana na viongozi wa ACT-Wazalendo, wananchi wa Zanzibar wameshirikiana na kupiga kasi ya maendeleo.

Alisema Uongozi wa Tume hiyo unafarijika na mafanikio makubwa yaliopatikana katika kipindi kifupi cha uongozi wa Dk. Mwinyi, pamoja na mambo mengine alimpongeza kwa kuimarisha na kutekeleza haki za binadamu pamoja na kukuza utawala bora.

Jaji Mwaimu alisema suala la kupokea malalamiko ya wananchi lipo katika ofisi nyingi za serikali na hatua yake ya kufungua milango na kusikiliza malalamiko ya wananchi yeye mwenyewe ni jambo jema linalolenga kuondokana na vikwazo vinavyoweza kujitokeza.

"Sisi utendaji wetu unazingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunahakikisha serikali inatetekeleza vizuri majukumu yake ili wananchi waweze kupata haki zao," alisema.

Alisema hatua ya Rais Dk. Mwinyi, kukutana na makundi mbalimbali ya kijamii, ikiwamo wazee na wenye ulemavu ni hatua nzuri katika kuendeleza utawala bora.

Jaji Mwaimu alimpongeza Dk. Mwinyi kwa juhudi zake za mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa pamoja na kuimarisha taasisi zinazosimamia suala hilo, na hatua zake za kuwawajibisha viongozi wasiozingatia utawala Bora.



Waziri wa Uwekezaji Zanzibar ambaye ni Mwakilishi wa Jimbo la Bububu, Mudrik Soraga (kulia) akijadiliana jambo na Mwakilishi wa Jimbo la Welezo, Hassan hafidh, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Chukwani, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Zanzibar yafanikiwa kutokomeza ndorobo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imefanikiwa kutokomeza wadudu aina ya ndorobo ambao walikuwa tishio kwa kushambulia mifugo ikiwamo ng'ombe.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema hayo wakati akitoa ufafanuzi wa mikakati ya serikali katika kupambana na wadudu waharibifu wanaoteketeza mazao ya mimea na mifugo.

Alisema ndorobo wameteketezwa moja kwa moja na sasa sio tishio kwa mifugo kutokana na juhudi za Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na shirika la mionzi ya nguvu za atomiki duniani ambalo ndiyo lililofadhili mradi huo.

Waziri huyo alisema kwamba serikali imejipanga kutekeleza mradi wa miaka minne wa kupambana na nzi wanaoharibu matunda ya wakulima na kusababisha mafunza.

"Zanzibar imepata mafanikio makubwa katika mradi wa kupambana na wadudu aina ya ndorobo ambao walikuwa adui mkubwa kwa mifugo ikiwamo ng'ombe na sasa tumejipanga kupambana na wadudu nzi wanaoharibu matunda na kusababisha wakulima kupata hasara kubwa," alisema.

Alisema katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021-2022, serikali imejipanga zaidi kuimarisha maabara za utafiti wa maradhi mbalimbali ikiwamo ya mazao ya mizizi, matunda pamoja na mifugo.

"Serikali imepokea malalamiko mbalimbali kutoka kwa wafugaji na wakulima kuhusu kuongezeka kwa maradhi yanayoshambulia sekta hizo na sasa imejipanga kufanya utafiti wa maradhi hayo," alisema.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamepitisha makadirio mapato na matumizi ya bajeti ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo jumla ya Sh. bilioni 53.70 na Sh. bilioni 17.18 kwa kazi za kawaida huku Sh. bilioni 2.75 zikitengwa kwa ajili ya kazi za utafiti.

# SMZ yaipa kipaumbele sekta ya uchumi wa bluu

**Na Rahma Suleima,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdallah, amesema kuwa Serikali ya Zanzibar imeipa kipaumbele sekta ya uchumi wa bluu unaoelekeza matumizi mazuri na endelevu ya rasilimali ya bahari ili wananchi waondokane na umasikini.

Aliyasema hayo wakati akifungua kongamano la maadhimisho ya miaka 40 ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), yaliofanyika Mjini Zanzibar.

Alisema ni muhimu katika majadiliano ya kongamano hilo kuonesha jinsi Zanzibar inavyoweza kutekeleza kipaumbele hicho na kuimarisha sekta ya uchumi wa bluu kupitia jumuiya hiyo.

Alisema wafanyabiashara kutoka Congo hufika Zanzibar kufanya biashara ya samaki na ni ushirikiano wa kiuchumi na kwamba ni vyema kuongeza ushirikiano huo na nchi zingine za SADC.

"Uzoefu unaonesha kuwa wafanyabiashara wetu wengi wanaelekeza macho yao Dubai, India au China tu... inawezekana kuna fursa nyingi za kibiashara katika nchi zetu za SADC ambazo tukizitumia vizuri Zanzibar itapiga hatua kubwa za kimaendeleo," alisema.

Vile vile, baadhi ya majirani wa Tanzania asilimia fulani ya uchumi inachangiwa na kuuza Kiswahili nje ya nchi na kwamba ni vyema ifike mahala Kiswahili kiwe ni rasilimali inayochangia katika kukuza uchumi wa nchi hasa ikizingatiwa kuwa makao makuu ya kamisheni ya Kiswahili ya Afrika yapo Zanzibar.

Alivitaka vyama, taasisi na vyombo vinavyoshughulikia maendeleo ya lugha ya Kiswahili kuazisha mijadala ya jinsi ya kutumia fursa za Kiswahili katika ukanda wa nchi za SADC na kisha kuyafanyia kazi mapendekezo ya mijadala hiyo.

Mwakilishi kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ambaye pia ni Mkurugenzi wa Mambo ya Nje Ofisi ya Zanzibar, Balozi Masoud Balozi, alisema tukio hilo adhimu na la kipekee linalenga kuenzi mchango mkubwa wa viongozi wakuu waanzilishi wa SADC ambao maono yao yaliweka msingi wa ukombozi kisiasa na kiuchumi kwa kanda ya Kusini mwa Afrika.

Alisema viongozi hao pia waliongeza uelewa wa wananchi kuhusu mtangamano wa SADC na faida ya uanachama wao husasan kuchangamkia fursa za kiuchumi ikiwamo uwekezaji na biashara.

Balozi huyo alisema wanapoadhimisha miaka 40 ya SADC hawawezi kuepuka kuzungumzia mchango mkubwa uliotolewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ni miongoni mwa nchi waanzilishi wa Jumuiya hiyo.

Alibainisha kuwa Tanzania ilikuwa mstari wa mbele kusaidia nchi za Afrika katika harakati za ukombozi hususan nchi za Kusini mwa Afrika chini ya uongozi wa hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye aliiletea heshima Tanzania kwa Bara la Afrika na ulimwenguni kwa ujumla.

Kwa Upande wake Makamu Mkuu wa chuo cha Taifa cha Zanzibar, Dk. Zakia Abubakar alishukuru Wizara ya Mambo ya Nje kwa kukichagua chuo cha Taifa Zanzibar kuwa mwenyeji wa kuandaa kongamano hilo.

Dk. Zakia alisema kufanyika kwa kongamano hilo katika chuo hicho kimetoa fursa ya kukitangaza zaidi chuo pamoja na kutoa fursa za kitaaluma kutoka SADC na kuahidi kuwa chuo cha SUZA kitakuwa mstari wa mbele katika kutekeleza majukumu yoyote yanayotolewa na serikali kwa lengo la kuleta maendeleo ya nchi.

Ujumbe wa mwaka huu unasema miaka 40 ya Jumuiya na Maendeleo ya Kiuchumi ya Mataifa ya Kusini na Mashariki wa Bara la Afrika ni kuimarisha amani, usalama na kuhamasisha maendeleo na ustahamilivu kati ya changamoto inayoikabili dunia.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**(JUDICIARY)**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA MOROGORO**
**MKOA MOROGORO**
**SHAURI LA USIMAMIZI WA MIRATHI NAMBA 4/2021**

**ALLEN SIKOMBE……………………MWOMBAJI**

**DHIDI YA MIRATHI YA**

**ALEX JOHNWELL SIKALUBA………MAREHEMU**

Mahakama hii inawafahamisha kwamba mwombaji wa kusimamia mirathi tajwa hapo juu amefungua shauri la kuomba usimamizi wa mirathi namba 4/2021 katika mahakama ya Wilaya Morogoro.


Shauri hilo limepangwa kutajwa mnamo tarehe 14 mwezi 06 mwaka 2021 saa 2:00 mbele ya Hakimu Richard Kasele asubuhi hivyo kwa yeyote mwenye pingamizi dhidi ya mwombaji afike katika Mahakama ya Wilaya Morogoro.

**Zingatia** kwamba kwa mpingaji yeyote ambaye hatofika tarehe hiyo, shauri litaanza kusikilizwa bila kutaarifiwa tena na maamuzi kutolewa.

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 25 mwezi wa 05 mwaka 2021

**HAKIMU MKAZI MFAWIDHI**
**MOROGORO**

## KUPOTEA KWA RESULTSLIP



**DARINI ABDALLAH RASHIDI** anatangaza kupotelewa na resultslip ya kidato cha nne yenye index namba **S4026/0023** iliyotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary BUNJU A.mwaka 2020,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/MAG/RB/241674/2021**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI NA.45 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**DEUSDEDITH MALENGO MATABA**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**ECHUMBA MISANGO ECHUMBA AND ERICK DEUSDEDITH MATABA**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(taarifa ya kawaida)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 15th mwezi june 2021
Imewasilishwa dar es salaam leo tarehe 11th mwezi wa may 2021

NAIBU MSAJILI

**JUDICIARY**
**IN DISTRICT COURT OF KASULU**
**TAXATION CASE NO 1/2021 ORIGINAL CIVIL CASE NO 5/2019 OF THE DISTRICT COURT OF KASULU IN KASULU DISTRICT**
**LAKE TANGANYIKA OIL COMPANY LIMITED**
**APPLICANT/DECREE HOLDER**
**BARNABAS ISSA MLANGA**
**VESUS**
**……..RESPONDENT/JUDGMENT DEBTOR**

**NOTICE OF HEARING.**
**TO BARNABAS ISSA MLANGA**
……………………………………………….

**TAKE NOTICE:** that the above mentioned appeal will be heard on 31st…….. day of May ……2021 AT 8:00 ….O'clock in his court you are therefore required to appear in the above mentioned date and time. Failure to do, hearing will proceed in your absence

Give under my hand and the seal of the court this 17th……….day of May 20 21

RESIDENT MAGISTRATE I/C

## KUFUNGWA KAMPUNI

Kampuni ya **SAMA SEA COMPANY LIMITED.** Iliyopo Dar es Salaam inatangaza kuifunga Kampuni yenye usajili **No.134047** uliofanyika tarehe 22/04/2017

**EDHA AHME DALI**
Mkurugenzi
**0688 223377**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GERVAS EPHRAIM MATOWO** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 181 AJD. ENGINE NO G16A392161. CHASSIS NO TDOIW211304.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. **TAARIFA YA POLISI –ARU/ARU/R-B/268047/2021.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**HILLARY HERMAN MOSHI**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji Yenye namba za usajili **MC 930 CSW.**
Yenye Chassis namba **MD5M14PA3L4KO7797** na Injini namba **AK4KL807642.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi Taarifa:
**MOS/TR/RB/468/2020**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI SHAHIDI**
**(MCA/84)**
**MAHAKAMA YA MWANZO MIKONGENI WILAYA YA MVOMERO**
**MIRATHI NAMBARI 07/2018**
**MUOMBAJI: JOHN S/O MARTINI CHAMZILA**
**MAREHEMU: MARTINI JONATHAN CHAMZILA**
**Kwa: JOHN S/O MARTINI CHAMZILA**
**MKAZI WA KISAKI MVOMERO**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba/Eleza hapa habari ya madai);
Unatakiwa kuhudhuri mahakamani Tarehe iliyopangwa hapo chini kwa ajili ya kuleta mgawanyo wa mirathi
Kwa hiyo nahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMATANO Tarehe 16/06/2021 saa 2:30 asubuhi/alasiri kwa mjibu. Madai hayo, na kuwa siku hiyo siku ya kutakwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wetu na hati zote zinahusu shauri hilo kwaajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shauri hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa. Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 26/05/2021

**Hakim wa Mahakama Ya Mwanzo**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

KINGLION INVESTMENT CO LIMITED ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 986 AVR AINA YA KINGLION.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/RB/268655/2021.

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI)**
**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA KATIKA MIRATHI NO.03/2021**
**MAREHEMU**
**MONICA JAMES KAZIMOTO**

Katika Mahakama ya Mwanzo **MAKANG`WA WILAYA CHAMWINO-DODOMA**
Usimamizi wa Mirathi **03/2021**

Ombi la **NICHOLAS JAMES KAZIMOTO** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **MONICA JAMES KAZIMOTO**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **01/07/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 21/05/2021**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MOSHI**
**WILAYA YA MOSHI**
**MAOMBI NA. 61/2020**

**YUSUF HAMIS LESSENGA**
**Msimamizi wa Mirathi ya Amina Ally**

**WALETA MAOMBI**
**SHEILA SADICK KAUNDA**
**JUMMY SADICK OMAR**

**DHIDI YA**

**ONESMO PAUL KIRIA**
**ALLY SADICK OMAR**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: ALLY SADICK OMAR, POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa waleta maombi wameleta maombi ya kesi na wameelezwa katika nakala ya madai ambayo inapatikana katika Baraza la Ardhi na Nyumba Moshi. Shauri limepangwa kusikilizwa tarehe 31/05/2021 saa mbili na nusu (2:30) asubuhi mbele ya Mheshimiwa Mwenyekiti P. J. Makwandi, hivyo unatakiwa kufika mahakamani wewe au mawakili wako .
**ANGALIA :** Kama hutahudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu Mahakama itasikiliza shauri hili na kutoa uamuzi upande mmoja .
Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 23 mwezi April , 2021.

**P.J .Makwandi**
**MWENYEKITI**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA MIRATHI**
**MIRATHI NA.21 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**SILVANUS AMBROSE BANDA**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**THEODORA ALFRED BANDA**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 29 mwezi wa june 2021
Imewasilishwa dar es salaam leo tarehe 26 mwezi may 2021.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

KISHAN ENTERPRISES LTD ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 282 BEX (SANYA). YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: DAR/KIJ/R-B/269865/2021.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BARIKIEL MOSSES SHAYO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye Namba za usajili **T 888 BGJ** aina ya Hummer. Chassis **No.5GTDN136968252602.** Engine **No.R68252602.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **TAARIFA YA POLISI: MAN/BAB/RB/268544/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DEBORA MUSA ILOMO** Wa Igomelo mjini Kahama, anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 254 DEC** aina ya **NISSAN.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake, Taarifa ya jeshi la polisi, **MAJ/RB/TR/719 /2021.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ISSA ABDUL OMARY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI FUSO** yenye namba za usajili **T 650 AMW** Lenye chassis namba **FK417J542640.** Injini namba **6D17749121.** KADI namba **8254603.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. Taarifa ya polisi RB. Namba: **IR/RB/2930/2021**

## U-FRESH FOOD LTD
## TAARIFA KWA UMMA



WAFANYAKAZI NA WATEJA WA **U-FRESH FOOD LTD** INAWATANGAZIA KUWA NDUGU, **JOSEPH PETER NTALE** MWENYE PICHA HAPO JUU ANATAFUTWA KWA MAKOSA YA WIZI AKIWA MTUMISHI WA **U- FRESH FOOD LTD,** KATIKA NAFASI YA MAUZO.KAMPUNI INAWAJULISHA SASA HAUSIKI NA KAZI ZOZOTE ZA KAMPUNI, WALA HATAMBULIKI KAMA MFANYAKAZI WA **U-FRESH FOOD LTD.** HIVYO BASI MNAONYWA KUTOSHIRIKIANA NAE KWENYE MASUALA YOYOTE YA KIOFISI.HIVYO BASI KAMPUNI INAOMBA KWA YEYOTE ATAKAE MUONA KUTOA TAARIFA KWA KAMPUNI AU KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU KWA KUMB: **RB NO BUZ/RB/67/2021.AU KWA KUPIGA SIMU NO 0757-666599/0758-966999/0763-658800.**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji

THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Ripoti: Wanawake wako nyuma katika uziduaji

**Na Mwandishi Wetu**

UTAFITI uliofanywa na Chuo Kikuu cha Mzumbe kuhusu jinsia na uziduaji, imebaini ushiriki wa wanawake katika uziduaji ni mdogo.

Akiwasilisha ripoti hiyo jijini Dar es Salaam jana wakati wa mjadala wa kitaifa wa jinsia na uziduaji, Mhadhiri wa chuo hicho, Dk. Mwajuma Kadilu, alisema kuwa wakati Sera ya Madini inatungwa mwaka 2000, ushiriki wa wanawake katika sekta hiyo ulikuwa wa asilimia 0.1.

Daktari huyo wa sheria alisema wamebaini kwa sasa ushiriki wa wanawake katika sekta hiyo ni chini ya asilimia tano.

Alibainisha vikwazo vingi vinavyosababisha hali hiyo vikijumuisha uteuzi usiozingatia jinsia serikalini wakiwamo makatibu wakuu, wanawake kutomiliki ardhi na kundi hilo kukosa mitaji, elimu na vifaa vya kuliwezesha kushiriki katika uziduaji.

Katika mapendekezo yao, Mzumbe waliishauri serikali na Bunge kufanyia kazi dosari hizo ili kuimarisha ushiriki wa wanawake kwenye sekta hiyo.

Awali, Mkurugenzi Msaidizi wa Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT), Rose Marandu, alisema kuna haja kutatua kikwazo cha unyanyasaji wa kijinsia, akidokeza baadhi ya wanawake wamekuwa wakinyanyasika kwa rushwa ya ngono wanapohitaji kupata zabuni na leseni za uchimbaji madini.

"Ipo dhana kwamba wanawake wanaokwenda migodoni wana lengo la kujiuza hata kama wanakwenda kwa nia ya kushiriki kwenye uchimbaji wa madini.

"Hili linarudisha nyuma ushiriki wa wanawake katika sekta hii kwa sababu wengi wanaingiwa na hofu hii ya kuonekana wanakwenda migodini kujiuza," alisema.

Mjadala huo ulioandaliwa na asasi ya HakiRasilimali, ulishirikisha wadau mbalimbali zikiwamo wizara, Mamlaka ya Mapato (TRA), Umoja wa Mataifa (UN), halmashauri zenye migodi ya madini, wabunge, madiwani na taasisi za elimu ya juu.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro (kushoto), akikata utepe kuzindua simu zitakazotumia kupokea taarifa za matukio ya wanyamapori kuvamia maeneo ya wananchi, jijini Dodoma jana, ambapo simu hizo wananchi watapiga bure. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# RC ataka majina w/biashara walioshindwa kulipa kodi

**Na Zuhura Zukheir,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, ameiagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Iringa kuwasilisha ofisini kwake majina ya wafanyabiashara walioshindwa kulipa madeni yao baada ya makubaliano ya kisheria.

Akizungumza kwenye kikao na wawakilishi wa wafanyabiashara na machinga wa mkoa huo, alisema kuwa hatawafumbia macho wafanyabiashara ambao tayari wamepewa agizo la kisheria kulipa madeni hayo, lakini wanakaidi kutoka kwa mamlaka husika.

Alimwagiza Meneja wa TRA Mkoa wa Iringa kupeleka majina na kukutana na wafanyabiashara hao wanaokimbia kulipa madeni yao licha ya serikali kuagiza kulipa.

Sendiga alisema wadaiwa hao wakilipa kodi inachangia katika kuboresha sekta mbalimbali kama miundombinu, afya, elimu, utalii, ardhi na kilimo katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo ya nchi.

Alisema akaunti za wafanyabiashara wakubwa wanaodaiwa madeni makubwa zilikuwa zimefungwa hapo awali na kufunguliwa kwa mujibu wa sheria na makubaliano ya TRA Mkoa wa Iringa kulipa madeni hayo ili waendelee na biashara kama ilivyokuwa awali.

"Ngoja niwaambie kuwa bila kulipa kodi nchi haiwezi kukuza uchumi wake wala haitaweza kuleta maendeleo kwa wananchi kwa wakati kwa kuwa itakuwa inakosa fedha za kuanzisha miradi mikubwa ambayo inafaida kwa serikali," alisema.

Aliitaka TRA kutoa elimu ya mlipa kodi mara kwa mara ili kuepusha wafanyabiashara kufunga biashara zao au kushindwa kulipa madeni ya kodi.

Akipokea maagizo hayo Meneja wa TRA mkoani humo, Lamson Tulyanje, alisema wamepokea agizo hilo na watalifanyia kazi ili kuwawezesha wafanyabiashara hao kufanya biashara kwa uhuru na kukuza mitaji yao.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa chemba ya wafanyabiashara wenye viwanda na kilimo wa mkoa huo, Edmund Mkwawa, alimwomba Mkuu huyo wa Mkoa atatue changamoto za wafanyabiashara ili kukuza mitaji yao.

Nao baadhi ya wawakilishi wa wafanyabiashara mkoa walimwomba Mkuu wa Mkoa kuacha kusikiliza majungu ya baadhi ya wafanyabiashara na kujikita kutatua changamoto walizomweleza kwa lengo la kukuza uchumi wa mkoa huo.

# Vipaumbele tisa Mifugo vyatajwa

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imeweka vipaumbele tisa kwa mwaka wa fedha 2021/22, huku ikiainisha vikwazo 13 katika kukuza sekta hizo.

Waziri Mashimba Ndaki alibainisha hayo jana alipowasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema utekelezaji wake utashirikisha wadau ili kuifikisha nchi kwenye uchumi wa viwanda kwa maendeleo ya watu.

Alivitaja vipaumbele hivyo kuwa ni kuimarisha ulinzi na usimamizi shirikishi pamoja na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi nchini, kudhibiti upotevu wa mapato ya serikali yatokanayo na sekta ya uvuvi.

Pia kuimarisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na sekta ya uvuvi, kuimarisha usimamizi wa rasilimali na uwekezaji katika ukanda wa uchumi wa bahari, kuimarisha usimamizi na uthibiti wa ubora, usalama na viwango vya samaki na mazao ya uvuvi.

Alisema wanakusudia kuimarisha miundombinu ya uvuvi na kukuza biashara ya mazao ya uvuvi, kuboresha upatikanaji wa taarifa na takwimu sahihi za uvuvi, kuimarisha utafiti, huduma za ugani na mafunzo ya uvuvi na kuongeza upatikanaji wa vifaranga na vyakula bora vya samaki.

VIKWAZO 13

Waziri huyo alibainisha vikwazo katika sekta ya uvuvi nchini kuwa ni uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi, uwekezaji mdogo katika uvuvi wa ukanda wa uchumi wa bahari na usindikaji wa mazao ya uvuvi.

Vingine ni ushiriki mdogo wa mamlaka za serikali za mitaa na wadau wengine katika kusimamia na kulinda rasilimali za uvuvi, kutopatikana kwa mikopo ya kutosha na yenye masharti nafuu kwa wavuvi na wakuzaji viumbe maji ikilinganishwa na mahitaji yao.

Pia uhaba wa maofisa ugani wa uvuvi na ukuzaji viumbe maji kulinganishwa na mahitaji ya wataalamu katika halmashauri, ukosefu na uchakavu wa miundombinu ya uvuvi hususan mialo ya kupokelea samaki na masoko.

Alisema kuna kikwazo cha uwezo mdogo wa rasilimali fedha wa kufanya utafiti mara kwa mara ili kutambua rasilimali zilizopo kwenye maji hususan katika ukanda wa uchumi wa bahari na kuendelea kuwapo kwa upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa.

Kuhusu Sekta ya Uvuvi, waziri huyo alisema maeneo ya kipaumbele ni kuimarisha afya ya mifugo, kuwezesha upatikanaji endelevu wa rasilimali za vyakula vya mifugo na maji kwa ajili ya mifugo na kuboresha kosaafu ya mifugo ili kuongeza tija na uzalishaji.

## KLINSMANN AUTAKA UKOCHA SPURS

**LONDON, England**

GWIJI wa Tottenham Hotspur, Jurgen Klinsmann amezungumza na Sky Sports kuhusu uwezekano wa kurudi kuinoa klabu hiyo kama mwenyekiti, Daniel Levy atampigia simu.

Spurs kwa sasa ipo kwenye sintofahamu kuhusu mshambuliaji wake, Harry Kane ambaye ameweka wazi kwamba, anataka kuondoka klabuni hapo baada ya michuano ya euro 2020.

Klinsmann, ambaye amekuwa nje ya kazi ya soka tangu alipoondoka kwenye mikoba ya kuinoa Hertha Berlin Februari mwaka jana, amebainisha kwamba, mara zote "anafikiria" kurudi Tottenham, ambako alifunga mabao 29 ya Ligi Kuu katika mechi 50 alizocheza katika vipindi viwili tofauti alivyokaa hapo.

Straika huyo wa zamani wa Ujerumani, ambaye alikuwa nahodha wa timu ya taifa kwenye michuano ya mataifa ya Ulaya mwaka 1996, ameonyesha wazi kwamba, anaweza kuchukua mikoba ya Jose Mourinho.

"Ilikuwa ni miaka ya kufurahisha wakati nikiwa pale Spurs," alisema Klinsmann akinukuliwa na Sky Sport.

"Kwa hakika ni ndoto yangu kurudi tena kuinoa Tottenham kama Levy atanipigia simu, nitakuwa tayari kwa moyo mmoja.

"Maisha ya soka la kisasa yanakwenda haraka sana, hivyo ni jambo muhimu kuangalia changamoto mpya wakati wowote inapotokea, hivyo nipo tayari kurudi tena."

## ZIDANE ANAJIANDAA KUONDOKA REAL MADRID

**MADRID, Hispania**

MAGAZETI ya nchini Hispania ya AS na Marca yote kwa pamoja yameripoti kwamba, Zinedine Zidane ataachia ngazi kama kocha wa Real Madrid.

Majaliwa ya Zidane hapo Real Madrid yameonekana kuwa kwenye sintofahamu baada ya kumaliza msimu wa 2020-21 bila taji lolote.

Madrid walimaliza wakiwa nafasi ya pili kwenye LaLiga, huku wakitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya nusu fainali na walitolewa kwenye Copa del Rey hatua ya 32.


Zidane alirudi kuwafundisha tena Los Blancos hao mwaka 2019, baada ya awali kuwanoa kuanzia mwaka 2016 hadi 2018, ambapo alishinda taji la Ulaya mara tatu mfululizo.

Na sasa mchezaji huyo wa zamani wa Ufaransa ameripotiwa kuwa yupo njiani kuondoka klabuni hapo baada ya uvumi wa siku kadhaa.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Zidane tayari ameshawaaga wachezaji wake na kuwaambia kwamba, hataendelea kuwapo katika kikosi hicho kwa msimu ujao.

Ripoti hiyo imedai kuwa, mabosi wa Madrid wamefanya mazungumzo na Zidane na kufikia makubaliano ya kuachana na kocha huyo jumla.





# CONTE AACHANA NA INTER MILAN

**MILAN, Italia**

ANTONIO Conte ameondoka Inter Milan kwa makubaliano ikiwa chini ya mwezi mmoja tangu atwae kombe la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, klabu hiyo imethibitisha.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 51 aliwasaidia Nerazzurri hao kutwaa kombe lao la kwanza la Scudetto tangu 2010 katika msimu wake wa pili klabuni hapo.

Conte, ambaye aliiongoza Inter kwenye fainali ya Ligi ya Europa kwenye msimu wake wa kwanza hapo San Siro, alikuwa na mwaka mwingine mmoja kwenye mkataba wake.

Hata hivyo, huku wamiliki wa klabu hiyo wakiwa kwenye mchakato wa kupunguza kwa mishahara ya wachezaji, ilithibitika Jumatano kwamba, Conte ataondoka kwenye nafasi hiyo.

Taarifa ya klabu hiyo ilisomeka: "FC Internazionale Milano inaweza kuthibitisha kwamba imefikia makubaliano na Antonio Conte kuvunja mkataba kwa maelewano.

"Klabu ingependa kumshukuru Antonio kwa kazi yake kubwa aliyofanya klabuni hapa, kuiwezesha Inter kubeba taji la 19.

"Antonio Conte atabakiwa kuwa sehemu ya historia ya klabu hii."

Majaliwa ya Conte yalianza kuwa shakani baada ya klabu hiyo kukumbwa na tatizo la kifedha lililotangazwa na mwenyekiti wake, Steven Zhang.

## HABARI MICHEZO



# EMERY
## SASA ATAKA LIGI YA MABINGWA ULAYA

**GDANSK, Poland**

UNAI Emery amesema kwamba, baada ya kutwaa taji lake la nne la Ligi ya Europa akiwa na Villarreal sasa analitaka kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Villarreal waliwafunga Manchester United kwa penalti 11-10 kwenye fainali ya Ligi ya Europa iliyopigwa Jumatano hapa Gdansk, baada ya kufungana bao 1-1 katika muda wa kawaida na ziada.

Gerard Moreno alianza kuiweka mbele Villarreal kabla ya Man United kusawazisha kupitia kwa nyota wake, Edinson Cavani.

Golikipa wa United, David de Gea alikosa penalti na hivyo kuifanya timu hiyo kutoka nchini Hispania kulitwaa taji hilo, likiwa ni kombe kubwa la kwanza kwa kipindi cha miaka 98.

Emery sasa ameweka rekodi ya kuwa kocha wa kwanza kushinda taji hilo mara nne akiizima ile ya Giovanni Trapattoni aliyeshinda mara tatu.

Na sasa Emery amebainisha kuwa baada ya mafanikio hayo anatamani kulibeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Najihisi fahari kwa kutwaa taji hili," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Tulikotoka hatukuonekana kama tumekuja kushinda taji la Ligi ya Europa, kwa sababu sio kazi rahisi.

"Walitaka mimi nifanye kazi yangu na kwa hakika kabisa nimeifanya na nimeweka historia yangu.

"Lakini tunaweza kutengeneza njia yetu kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya."

## LUKAKU NAYE KUSEPA INTER MILAN

**MILAN, Italia**

ROMELU Lukaku anatarajiwa kufanya maamuzi kuhusu majaliwa yake Inter Milan mara tu atakapoteuliwa mrithi wa Antonio Conte klabuni hapo.

Kuondoka kwa Conte klabu hapo kumeongeza uwezekano wa Lukaku kuondoka kwa mabingwa hao wa Serie A kipindi hiki cha majira ya joto.

Lukaku amekuwa na furaha tangu ajiunge hapo Inter, lakini Conte alikuwa sababu ya yeye kukubali kutua hapo akitokea Manchester United miaka miwili iliyopita na klabu kadhaa ikiwamo Chelsea zimeonyesha nia ya kuitaka saini yake.

Conte aliondoka Milan Jumatano baada ya kuambiwa na uongozi wa Inter kuwa anahitaji kukata bajeti ya euro milioni 100 kwa ajili ya msimu ujao, na kocha huyo wa zamani wa Chelsea mikoba yake inaweza kuchukuliwa na kocha wa sasa wa Lazio, Simone Inzaghi.

Inter ilimsajili Lukaku kwa pauni milioni 74 na ameonyesha thamani yake baada ya kuifungia timu hiyo mabao 64 katika misimu miwili.

Amebakiwa na miaka mitatu kwenye mkataba wake wa sasa hapo Inter na kwa sasa yupo likizo wakati akisubiria kwenda kwenye michuano ya euro 2020 akiwa na kikosi cha Ubelgiji.

Lukaku na Inter watasubiri kwanza kuteuliwa kwa kocha mwingine kabla ya kuamua majaliwa yake.

## DONNARUMMA ATAONDOKA MILAN – MALDINI

**MILAN, Italia**

PAOLO Maldini amethibitisha kwamba, golikipa, Gianluigi Donnarumma ataondoka AC Milan kama mchezaji huru.

Majaliwa ya kipa huyo wa Italia yamekuwa kwenye sintofahamu kwa muda mrefu baada ya kuonesha nia ya kutotaka kusaini mkataba mpya, ambapo wa sasa unamalizika mwishoni mwa mwezi huu.

Mkurugenzi wa Milan, Maldini amebainisha kwamba, kipa huyo mwenye umri wa miaka 22 anaondoka kwa miamba hao wa Serie A.

"Nafikiri tunatakiwa kuwashukuru wachezaji wote kwa mchango wao katika msimu huu wa kuvutia," alisema Maldini akinukuliwa na Sky Sport.

"Gigio alikuwa kiongozi na mara kwa mara nahodha. Watu wakati mwingine huwa hawajui nini maana ya soka la kulipwa, kwani mambo yanabadilika wakati wowote kutegemea na maamuzi ya mchezaji mwenyewe.

"Ni ngumu kukubali, lakini ni ngumu kwake kuendelea na timu hii kwani ana matarajio yake mengine, lakini ni ngumu pia kukaa kwa muda mrefu na timu moja.

"Tunatakiwa kuwaheshimu wale wote walioipa Milan mambo mazuri na Donnarumma tutamkumbuka mara kwa mara kwa uwezo wake."

Donnarumma amekuwa akihusishwa na timu kama Juventus, Barcelona na Manchester United.

Na golikipa wa Lille, Mike Maignan anaripotiwa kwamba anaweza kuchukua nafasi ya Donnarumma pale kwenye dimba la San Siro.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER: MAN UNITED HAIKUWA KWENYE UBORA

●●●Asema sasa wanajipanga kwa msimu ujao, na amekubali kuwa hawakuwa na...

**GDANSK,** Poland

OLE Gunnar Solskjaer amekubali Manchester United "haikuwa kwenye ubora" na msimu wao haukuweza kuwa wa mafanikio baada ya kufungwa na Villarreal kwenye fainali ya Ligi ya Europa.

David de Gea alikosa penalti kwenye mchezo huo uliokuwa na changamoto ya kupigiana matuta mengi katika uwanja wa Gdansk nchini Poland, ambapo Villarreal walishinda taji lao kubwa la kwanza la Ulaya, juzi Jumatano usiku.

Golikipa wa United, De Gea alishindwa kufunga penalti hiyo na kuwafanya Villarreal kuibuka na ushindi wa penalti 11-10, baada ya timu hizo kutoka sare ya kufungana bao 1-1 katika muda wa kawaida na ule wa ziada.

Gerard Moreno alianza kuwaweka mbele vijana hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, katika kipindi cha kwanza likiwa ni bao lake la 30 msimu huu na la 82 kwa klabu hiyo, akifikia rekodi iliyowekwa na Giuseppe Rossi ya mabao 82.

Edinson Cavani alisawazisha dakika 10 bada ya kipindi cha pili, lakini United walishindwa kupata taji lao la kwanza chini ya Solskjaer.

Unai Emery, kwa upande mwingine, amekuwa kocha wa kwanza kushinda taji la Ligi ya Europa mara nne, akiizima ile ya Giovanni Trapattoni, aliyeshinda mara tatu.

Solskjaer anajua kwamba mashetani wekundu hao hawakuwa wazuri kutosha kuweza kupata mafanikio makubwa msimu huu, na sasa anaungalia zaidi msimu ujao.

Kocha huyo raia wa Norway aliiambia BT Sport baada ya mchezo huo: "Kwa kifupi inakatisha tamaa kwenye vyumba vya kubadilishia nguo.

"Soka ndivyo lilivyo. Wakati mwingine matokeo yanaamuliwa na mkwaju mmoja na wakati mwingine mambo yanakuwa tofauti kabisa.

"Tunatakiwa kujifunza kutokana na hilo, sio hisia nzuri kwa sasa na nina uhakika hatutarudia tena makosa kama haya.

"Hatukuwa kwenye ubora. Hatukucheza vizuri na tunajua kwamba tunaweza. Tulianza vizuri na wao haraka wakapata bao. Tulikatishwa tamaa na bao lile.

"Tulijaribu kusukuma mashambulizi mbele na kapata bao la kusawazisha. Baada ya kufunga hatukuweza kutawala mchezo kama tulivyotaka. "Tulikuwa na nafasi nyingi, lakini tulishindwa, wao walilinda vizuri zaidi lango lao. Hatukutengeneza nafasi nyingi za kufunga."

## KWA UFUPI

**ZIDANE SASA KUONDOKA**

KOCHA Zinedine Zidane ameamua kuondoka Real Madrid na tayari ameshawafahamisha wachezaji juu ya uamuzi wake huo siku ya Jumatano. (*AS*)

**SOUMANRE SAFI LEICESTER**

LEICESTER City wanakaribia kukamilisha makubaliano ya usajili wa pauni milioni 18 wa kiungo wa mabingwa wa Ligi ya Ufaransa, Lille, Boubakary Soumare mwenye umri wa miaka 22. (*Sky Sports*)

***

**ABRAHAM NA HUDSON-ODOI**

KLABU ya Borussia Dortmund inafanya mawasiliano na Chelsea juu ya uwezekano wa kuwasajili Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 23 na Callum Hudson-Odoi mwenye miaka 20. (*90min*)

**WEST KUMKOSA TAMMY**

WEST Ham huenda wasiweze kufikia kiwango cha pauni milioni 40 ambacho Chelsea wanakitaka kwa ajili ya usajili wa Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 23. (*TeamTalk*)

**SANCHO NJIA NYEUPE**

NIA ya Dortmund ya kumtaka Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 20 inaweza kutoa fursa kwa mshambuliaji wa England, Jadon Sancho mwenye miaka 21 kuondoka katika klabu hiyo ya Bundesliga kuelekea Manchester United. (*Mirror*)

**KONATE TAYARI LIVERPOOL**

LIVERPOOL wamefikia makubaliano ya kumsajili beki wa Ufaransa, Ibrahima Konate mwenye umri wa miaka 22, kutoka klabu ya RB Leipzig kwa mkataba wa miaka mitano. (*ESPN*)

**DE PAUL KUTUA LIVERPOOL**

MATUMAINI ya Liverpool kumsajili kiungo wa Udinese, Rodrigo de Paul mwenye umri wa miaka 27 raia wa Argentina yameongezeka baada ya AC Milan kuachana na mpango wa kutaka kumsajili. (*Express*)

**RAPHINHA HANA MPANGO**

WINGA wa Brazili, Raphinha mwenye umri wa miaka 24, amesema kuwa hafikirii kuhusu kuondoka Leeds United, licha ya tetesi zinazomuhusisha na kuhamia katika klabu za Manchester United na Liverpool. (*Metro*)

**COUTINHO KUSUBIRISHWA**

KLABU za Ligi Kuu England zitatakiwa kusubiri hadi Julai kabla ya kuwasiliana na Barcelona kuhusu mipango ya kumsajili kiungo mshambuliaji wa Brazil, Philippe Coutinho mwenye umri wa miaka 28. Arsenal na Everton wanadhaniwa kuwa wanamtaka. (*Sky Sports*)

**JOHNSTONE NA HATIMA**

GOLIKIPA wa England, Sam JOHNSTONE mwenye umri wa miaka 28, amesema mustakabali wake upo mikononi mwa klabu ya West Brom licha ya kuhusishwa na taarifa za kuhamia Leeds na West Ham kwa malipo ya pauni milioni 20. (*Mail*)

**INZAGHI KUMRITHI CONTE**

KOCHA wa Lazio, Simone Inzaghi anaweza kuchukua nafasi ya Antonio Conte kuinoa Inter Milan. Conte ameamua kuondoka Inter kwa kuwa uongozi wa klabu hiyo unataka kuacha wachezaji wenye thamani ya euro milioni 80 ili kukabiliana na ukata wa kifedha. (*Sky Sports*)

HABARI MICHEZO

# BIASHARA UNITED YAANZA MIKAKATI 'KUIUA' YANGA

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Biashara United umesema timu yao itaandaa programu 'maalumu' kwa ajili ya kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mchezo wa nusu fainali wa mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Yanga ili wasonge mbele katika michuano hiyo, imefahamika.

Biashara United ilitinga hatua hiyo baada ya kuwafunga Namungo FC mabao 2-0 kwenye mechi ya robo fainali sawa na ushindi ambao Yanga walipata walipocheza na Mwadui FC mkoani Shinyanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Biashara United, Selemani Mataso, alisema wanatarajia kuingia kambini mapema wiki ijayo baada ya kocha wao, Patrick Odhiambo kurejea nchini akitokea kwao Kenya alipokwenda kuisalimia familia yake.

**"Wiki ijayo ndio tutaanza mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kukutana na Yanga kwenye mchezo wetu wa nusu fainali ya FA, lengo letu ni kuingia kwenye fainali ya mashindano hayo na tunawaomba mashabiki wetu wazidi kutuunga mkono ili tusonge mbele," alisema Mataso.**

Kiongozi huyo alisema tayari kocha wao ameshabaini mapungufu ya kikosi chake na ameandaa mbinu mpya ili kuwaimarisha wachezaji wake kwa sababu wanahitaji kumaliza msimu huu na mafanikio.

Kuhusu suala la usajili alisema wana mpango wa kuongeza wachezaji ndani kwa ajili ya kuongeza nguvu kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano mengine watakayoshiriki.

"Baada ya kumaliza michezo yetu iliyobakia, kocha atatoa ripoti yake na baada ya kuipitia tutajua anahitaji wachezaji wangapi kwa ajili ya msimu ujao na anaacha wachezaji wangapi, tunaomba mashabiki wetu waendelee kuwa wavumilivu," Mataso alisema.

Mwenyekiti huyo aliongeza kwa sasa wataendelea kupambana kwa kutumia wachezaji waliopo ambao wanaamini wamekuwa na msimu mzuri tofauti na misimu mingine iliyopita.

"Msimu huu umekuwa na ushindani sana, lakini tumefanikiwa kupambana na leo hii tuko katika nafasi za juu, ingawa malengo yetu yalikuwa ni kuwania ubingwa, naamini tutajiimarisha ili kufanya vizuri zaidi msimu unaofuata," aliongeza kiongozi huyo.

Biashara United yenye pointi 45 iko katika nafasi ya nne ikiwa imecheza mechi 30, imeshinda michezo 12, sare tisa na imepoteza michezo tisa.



Wachezaji wa Timu ya vijana ya Yanga maarufu Yanga B, wakiwa katika mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Chuo cha Sheria na Mawasiliano kilichoko jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Selous Marathon kufanyika Agosti

**Na Mary Geofrey**

WANARIADHA mbalimbali kutoka ndani na nje ya Tanzania wanatarajiwa kushiriki katika mbio za Selous 'Selous Marathon 2021' ambazo zinatarajiwa kufanyika ifikapo Agosti 21, mwaka huu mkoani Morogoro, imeelezwa.

Akitangaza kuanza kwa mbio hizo jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano, Imani Kajura, alisema mwaka huu mbio hizo zimepangwa kufanyika kwa awamu ya pili.

Kajura alisema lengo la kuandaa mbio hizo ni kuendelea kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo hapa nchini kupitia kwa wanariadha mbalimbali ambao watakutana Morogoro kuchuana na kuitaja kauli mbiu ya mwaka huu ni 'Selous Marathon, Na Mimi Nimo'.

"Mbuga ya Selous ni kubwa ipo katika mikoa zaidi ya mitatu, hivyo sisi tumeona tufanye mashindano hayo katika eneo la Morogoro ambako ni sehemu ya mbuga hii ili kutangaza utalii wetu na kuwabadilishia mazingira wanamichezo waliozoea kukimbia mikoa mingine," alisema Kajura.

Aliongeza kutakuwa na bima ya maisha kwa wanariadha watakaoshiriki ambayo itakuwa na thamani ya Sh. milioni tano endapo mshiriki atapoteza maisha, pia bima ya ulemavu ya Sh.milioni nne na bima ya Sh. milioni moja kwa mshiriki atakayeumia.

Naye Ofisa Mkuu Utawala wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Jacob Nduye, aliwataka Watanzania kushiriki mbio hizo zenye lengo la kutangaza utalii, kujenga afya ya mwili na kujumuika pamoja watu kutoka maeneo mbalimbali.

Nduye alisema mbio hizo zimepata baraka kutoka serikalini na wanaamini zitachangia katika kukuza na kuendeleza vipaji vya wanariadha wa hapa nchini.

# Tumekosa magoli mengi - Azam FC

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya timu yake kusonga mbele katika mashindano ya Kombe la FA ambayo yameingia hatua ya nusu fainali, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema iwapo washambuliaji wake wangekuwa na utulivu wangeondoka uwanjani na ushindi mnono.

Azam FC imetinga hatua ya nusu fainali baada ya kuwafunga Rhino Rangers mabao 3-1, katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kambarage mkoani Shinyanga juzi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Vivier alisema mechi yao hiyo ilikuwa na ushindani mkubwa hasa katika kipindi cha kwanza ambacho wapinzani wao walikuwa fiti zaidi na wao walishindwa kutumia vizuri nafasi walizotengeneza.

Vivier alisema kipindi cha kwanza washambuliaji wao hawakuwa na utulivu hali ambayo inawafanya kupoteza nafasi nyingi za kufunga lakini kama wangetumia vyema, wangeibuka na ushindi wa mabao mengi.

"Kama nilivyosema tangu mwanzo kuwa mchezo utakuwa mgumu. Na kweli ulikuwa mgumu. Kwa sababu wakati sisi tukipoteza nafasi Rhino walikuwa na uwezo wa kuuchezea mpira na mpaka wakafanikiwa kutufunga. Ilibidi tufanye kazi ya ziada kukomboa goli na kufunga mengine mawili," alisema Vivier.

Alisema kuwa Rhino walipata bahati kwa sababu wao hawawafahamu vizuri, huku Azam yenyewe ikiwa inafahamika uchezaji wao.

# Mafunzo yajipanga kuichapa Mlandege

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BENCHI la Ufundi la Mafunzo limesema bado timu yao ipo katika mbio za kuusaka ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu ambao unaelekea ukingoni.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar, Mafunzo ipo kwenye nafasi ya pili ikiwa na pointi 32 wakati vinara wa ligi hiyo ni KMKM yenye pointi 37 na timu zote zimebakisha michezo mitatu ili kumaliza msimu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Mafunzo, Said Kwimbi kuelekea mchezo wake dhidi ya Mlandege utakaochezwa leo alisema matarajio yake kuondoka na pointi tatu ili kujiimarisha katika safari yao ya kutwaa ubingwa wa ligi hiyo.

Kwimbi alisema licha ya kuzitaka alama tatu katika mchezo wake wa leo, anaamini mchezo huo hautakuwa rahisi kama unavyodhaniwa kwa sababu Mlandege nayo inahitaji kushinda ili kujitoa katika mstari wa hatari wa kushuka daraja.

Alisema amewaandaa wachezaji wake kutumia vyema nafasi watakazopata pamoja na kufanya uamuzi sahihi pale wanapotengeneza nafasi za kufunga.

"Tatizo kubwa lililopo kwa wachezaji ni kushindwa kuwa na maamuzi ya haraka pale wanapopata nafasi ya kupenya katika lango la wapinzani, nimewafundisha mbinu ya kutumia akili zaidi ili tuweze kupata magoli ya mapema," alisema Kwimbi.

Aliongeza licha ya Mlandege kutokuwa katika nafasi nzuri katika msimamo wa ligi, anafahamu ina kikosi kizuri na anatarajia kukutana na ushindani katika dakika zote 90 za mchezo huo.

# Michezo

Ijumaa Mei 28, 2021
Nipashe



SOLSKJAER: MAN UNITED HAIKUWA KWENYE UBORA HABARI UK 22




Meneja Maendeleo ya Biashara na Miradi wa Kampuni ya Jackson Group Sports, Levis Paul (katikati), akiwatambulisha mabondia Hassan Mwakinyo wa Tanzania (kulia) na Antonio Mayala kutoka Angola ambao watapanda ulingoni kuwania ubingwa wa Afrika wa uzito wa Super Welter katika pambano litakalofanyika leo kwenye Ukumbi wa Next Door Arena, Masaki jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# GOMES AWAKUBALI WACHEZAJI SIMBA

## ●●●Awaambia kazi iendelee mpaka pale watakapotetea ubingwa wa FA pamoja...

**Na Saada Akida**

MKO vizuri! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes baada ya timu yake kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Dodoma Jiji FC na kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA ambayo bingwa wake ataiwakilisha Tanzania Bara kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kwa ushindi huo wa juzi, Simba itakutana na Azam FC utakaochezwa kati ya Juni 24 na 28 mwaka huu mjini Songea na mchezo mwingine wa hatua ya nusu fainali utawakutanisha Biashara United na Yanga kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora.

Akizungumza na gazeti hili jana, Gomes alisema anajivunia sana kazi ya kujituma inayofanywa na wachezaji wake lakini amebainisha bado anahitaji kuboresha mbinu kuelekea hatua inayofuata ya michuano hiyo.

Gomes alisema ana wachezaji ambao wanajituma sana katika kila mechi hali ambayo wamefanikiwa kupata ushindi dhidi ya wapinzani wao Dodoma Jiji ambao mara zote wanapokutana wanawasumbua.

Kocha huyo alisema baada ya kufanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali sasa wanajipanga kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo uliokuwa mbele na hatimaye kutinga fainali ya michuano hiyo kwa mara ya pili mfululizo.

"Kila tunaposonga mbele katika michuano hii inazidi kubwa migumu na ushindani unakuwa mkubwa, tunatakiwa kusahau matokeo ya mechi hii na sasa kuangalia mechi yetu ijayo ambayo nina imani itakuwa nzuri na yenye mvuto kutokana na malengo ya pande zote mbili, kwetu na wapinzani wetu."

"Tunajua mchezo wa nusu fainali utakuwa ngumu, Azam wanataka kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao na huku ndiko wanaona kuna nafasi zaidi, lakini sisi lengo letu ni kufika fainali na hatimaye kutetea ubingwa wetu," alisema Gomes.

Aliongeza anarekebisha makosa yaliyojitokeza katika mchezo huo wa juzi, pamoja na kuwakumbusha washambuliaji wake kuwa na utulivu wa kutumia vyema nafasi wanazozitengeneza kwa ajili ya kujiandaa na michezo iliyopo mbele yao.

Naye Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji FC, Mbwana Makata, ameipongeza Simba kwa kufanikiwa kusonga mbele na ana imani walistahili kwa sababu ya ubora waliokuwa nao.

Makata alisema anakubaliana na matokeo waliyopata katika mchezo huo wa robo fainali na kuwapongeza wachezaji wake kupambana na kufuata maelekezo aliyowapa lakini ubora wa wapinzani wao uliwamaliza.

"Tumetolewa na timu bora, Simba ni bora kwa sasa, sisi ni mara ya kwanza kufika hatua hii, tumejifunza na tunaenda kujiandaa kwa ajili ya msimu ujao," alisema Makata.

Fainali ya michuano hiyo itafanyika Julai 25, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma na Simba ndio mabingwa watetezi ambao waliifunga Namungo FC ya Lindi mabao 2-1.

# UCHAGUZI WA TFF MAMBO YAMEIVA

**Na Mwandishi Wetu**

UCHAGUZI Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), unatarajia kufanyika ifikapo Agosti 7, mwaka huu, imefahamika.

Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema tarehe hiyo ya uchaguzi imepitishwa katika kikao cha Kamati ya Utendaji ya shirikisho hilo kilichofanyika jijini Dar es Salaam jana.

Karia alisema kikao hicho pia kilipokea ripoti na taarifa mbalimbali za maendeleo, marekebisho na maboresho ya kanuni yaliyowasilishwa na Kamati ya Sheria.

"Tumekutana katika kikao cha kikatiba cha kawaida, tumeongelea pia kuhusu masuala ya miradi ya Kigamboni (Dar es Salaam) na Tanga,...lakini tumepitisha tarehe ya mkutano mkuu, na tarehe hiyo tutampelekea Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ili na yeye ataendelea na taratibu zake, kwa sababu katika mkutano mkuu agenda mojawapo ni uchaguzi," alisema Karia.

Uchaguzi huo wa TFF unafanyika baada ya viongozi walioko madarakani ambao walichaguliwa Agosti 12, mwaka 2017, kumaliza muda wao wa miaka minne kwa mujibu wa katiba.

Tayari mikoa imeshafanya chaguzi zake za kupata wawakilishi watakaohudhuria mkutano huo na sasa ni wakati wa vyama shirikishiki kimojawapo ni Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Tanzania (TWFA), kitakachopata viongozi wake wapya ifikapo Juni 26, mwaka huu.

Usaili kwa ajili ya wagombea wanaowania nafasi mbalimbali za uongozi wa TWFA unatarajiwa kufanyika kesho Jumamosi jijini Dar es Salaam na muda wa kampeni kwa watakaopitishwa ni kuanzia Juni 18 hadi 25, mwaka huu.

Nafasi ya Mwenyekiti inawaniwa na Amina Karuma pamoja na Sarah Chao wakati Roseleen Kissiwa na Beatrice Mgaya wanachuana katika nafasi ya Makamu Mwenyekiti huku Somoe Ng'itu akiwa mgombea pekee katika nafasi ya Katibu Mkuu sambamba na Veronica Samo anayewania nafasi ya Katibu Msaidizi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002